Jumatatu Januari 4, 2021 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

# Nipashe

ISSN 0856 • Na. 0580450

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper LIKE & FOLLOW US



**Askofu** alaani biashara usafirishaji binadamu

UKURASA 15



**BAVICHA** yaja na mkakati kudai katiba mpya...

UKURASA 18

**Zidane amgeukia Benzema, amtaja Hazard**

UKURASA 21

# Sakata ucharazaji bakora latua kwa AG

UKURASA 2



Waziri wa Mambo ya Ndani, George Simbachawene, akiwajulia hali baadhi ya majeruhi wa ajali ya treni iliyotokea eneo la Kigwe-Bahi waliolazwa katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Dodoma jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Adaiwa kumuua kaka yake kwa deni la 13,000/-

UKURASA 2

## Ajali ya treni ilivyoua 3

UKURASA 2

**MICHEZO** NAMUNGO YAWAFUATA WASUDAN UK.23 | MAONI, KATUNI UK.6

# Ajali ya treni ilivyoua watatu

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

ABIRIA watatu wamefariki dunia na wengine 66, kujeruhiwa katika ajali iliyotokea juzi jioni maeneo ya Kigwe, wilayani Bahi, mkoani Dodoma, baada ya treni iliyokuwa na abiria 720 kupinduka na mabehewa kadhaa kuanguka baada ya njia ya reli kubomoka kutokana na mvua kubwa inayonyesha eneo hilo.

Taarifa iliyotolewa na Shirika la Reli Nchini (TRC), treni iliyosababisha vifo hivyo ilikuwa inatoka Dar es Salaam kuelekea mikoa ya Tabora, Kigoma, Mpanda na Mwanza.

Akizungumza katika eneo la ajali baada ya kufanya ziara ya kukagua, Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, George Simbachawene, alisema moja ya chanzo cha ajali hiyo ni mvua kubwa inayoendelea kunyesha hivi sasa na kusababisha mchanga pamoja tope kufunika njia ya treni.

Aidha, Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Dk. Binilith Mahenge, akizungumzia tukio hilo alitaja mvua kubwa iliyonyesha katika eneo hilo la Kigwe ilizoa msingi wa reli na kuisababisha kukosa nguvu na hivyo kuwa chanzo cha ajali hiyo.

"Mvua kubwa sana imenyesha katika eneo lile hali ambayo imesababisha msingi wa reli kuondolewa na maji na kusababisha reli kuinuka juu ndiyo hofu yetu kuwa reli haikuwa na nguvu ya kuhimili mzigo na kusababisha ajali hii," alifafanua Dk. Mahenge.

Alisema zaidi ya abiria 400, walisafirishwa na mabasi wakati zaidi ya 20 walipelekwa Manyoni kuendelea na safari katika mikoa waliyokuwa wanaelekea na watu wote wameshaondolewa kwenye sehemu hiyo, kazi iliyobaki ni kunyanyua mabehewa na mitambo imeshaandaliwa kufanyakazi hiyo.

Katika taarifa iliyotolewa na Kitengo ya Mawasiliano cha TRC, treni hiyo iliwasili jijini Dodoma juzi saa 9:15 alasiri na kuondoka saa 11:40 jioni kuelekea mikoa ya Tabora, Shinyanga, Kigoma, Mwanza na Mpanda.

Taarifa hiyo ilisema iliwasili saa 12:25 jioni katika stesheni ya Kigwe wilayani Bahi na kuondoka saa 12:27 kuendelea na safari, lakini ikapata ajali. Aidha, ilieleza kuwa ajali hiyo ilihusisha treni B 17, yenye mabehewa 12 na abiria 720.

Ilisema mabehewa sita kati ya 12 yalipinduka na kusababisha vifo vya watu watatu akiwamo mtoto mmoja na wanawake wawili na majeruhi 66 ambao wamefikishwa katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Dodoma (General Hospital) huku wengine wakiendelea na matibabu katika Hospitali ya Bahi.

Taarifa hiyo iliyosainiwa na Mkuu wa kitengo hicho cha mawasiliano cha TRC, Jamila Mbarouk, ilisema uchunguzi wa chanzo cha ajali hiyo unaendelea kufanyika na shirika litatoa taarifa ya tukio hilo.

Wakati huohuo, jana asubuhi Makamu wa Rais, Samia Suluhu Hassan, alitembelea majeruhi wa ajali hiyo waliolazwa katika Hospitali ya Mkoa wa Dodoma.

Akiwa hospitalini hapo aliushukuru uongozi wa mkoa wa Dodoma, Shirika la Reli pamoja na Wizara ya Afya pamoja na Mganga Mkuu wa Serikali kwa ushirikiano walioonyesha kuhakikisha majeruhi wote wanapata matibabu.

Makamu wa Rais alitembelea wodi nne na kuona majeruhi hao wanaendelea vizuri, huku wale waliovunjika mikono na miguu tayari wamefanyiwa upasuaji na kuendelea na kutibiwa hospitalini hapo.

Aidha, Makamu wa Rais, alisema TRC kwa kushirikiana na uongozi wa mkoa itasimamia kuhakikisha wagonjwa hao watakaporuhusiwa wanapatiwa usafiri wa kuelekea katika mikoa yao.

Halikadhalika, Mganga Mkuu wa Serikali Prof. Habel Makubi, alisema wamepokea majeruhi 65 na wengine 25 walibaki Hospitali ya Bahi kuendelea na matibabu, kutokana na hali zao kuwa nzuri.

# Sakata ucharazaji bakora latua kwa AG

**Na Thobias Mwanakatwe**

SAKATA la mfululizo wa viongozi kuwacharaza bakora wananchi limefikishwa katika Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali (AG), Profesa Adelardus Kilangi na kuahidi kulifanyia kazi.

Suala hilo lilifikishwa mwishoni mwa wiki kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali baada ya mwananchi mmoja kutoka Mtwara kupiga simu katika kipindi cha runinga cha Papo kwa Papo na kuhoji uhalali wa viongozi kutandika watu viboko hadharini.

Akitoa hoja yake katika kipindi hicho kinachoendeshwa na Katibu wa Itikadi na Uenezi wa CCM, Humphrey Polepole, msikilizaji huyo alisema kumekuwa na mfululizo wa viongozi kuwadhalilisha wananchi kwa kuwacharaza bakora jambo alilodai ni kinyume cha sheria.

Kufuatia malalamiko ya mwananchi huyo, Polepole alimpigia simu Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Prof. Kilangi, kupata ufafanuzi wa kisheria kuhusu jambo hilo.

Prof. Kilangi akijibu malalamiko hayo alisema, suala la wananchi kupigwa bakora na viongozi amelisikia na wapo baadhi ya wananchi ambao wamemfikishia malalamiko hayo.

"Katika hili niseme tumelipokea rasmi na tutalifanyia kazi kwa mujibu wa utaratibu kama tulivyokabidhiwa kikatiba na sheria zilizotungwa na bunge," alisema Prof. Kilangi.

Aidha, Prof. Kilangi alisema ofisi ya AG wajibu wao ni kutoa ushauri wa kisheria kwa serikali, viongozi na taasisi mbalimbali kuhusu tafsiri ya sheria au kueleza sheria inasema nini katika jambo fulani.

Alisema wanapotoa ushauri wa kisheria kwa jambo fulani huwa hawaelezi, lakini hatua huchukuliwa na changamoto inakuwa ni uelewa wa sheria inasemaje au inatafsiri nini.

Tamko hilo la Mwanasheria Mkuu wa Serikali limekuja baada ya wiki iliyopita Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu anayeshughulikia watu wenye ulemavu, Ummy Nderiananga, kuwacharaza viboko watu waliodaiwa kudhalilisha wenye ulemavu jijini Dar es Salaam kwa kuwatembeza mitaani kuwa ombaomba.

Katika tukio lingine kama hilo, Mkuu wa Wilaya ya Arusha, Kenani Kihongosi, aliwacharaza viboko wanafunzi watatu wa kidato cha kwanza wa Sekondari ya Sinoni pamoja na wananchi wengine kwa tuhuma za kuiba viti 108 vya shule hiyo.

Pia Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila, Oktoba 2019 aliwacharaza viboko na kuwaondoa shuleni wanafunzi wa kidato cha tano na sita wa Sekondari ya Kiwanja iliyopo wilayani Chunya kwa madai ya kuchoma mabweni.



Baadhi ya wananchi wa Kijiji cha Nadonjoki wanaolalamikia makazi yao kubomolewa kutokana na mgogoro wa mpaka wa kijiji chao na cha Terati Wilaya ya Simanjiro, wakiwa wamekaa na watoto wao katika eneo hilo, linalodaiwa kuwa na mgogoro wa muda mrefu. **PICHA: ASIRAJ MVUNGI**

# Adaiwa kumuua kaka yake kwa deni la 13,000/-

**Na Dege Masoli**, KILINDI

MKAZI wa Kitongoji cha Kwesalaka wilayani Kilindi, mkoani Tanga, Seif Hatibu, anatuhumiwa kumuua kaka yake Mahimbo Hatibu kwa madai ya ugomvi wa deni la Sh. 13,000.

Tukio hilo lilitokea juzi saa 1:30 usiku na inadaiwa kuwa Mahimbo alikwenda kwa Seif ambaye ni mdogo wake, kumdai kiasi hicho cha fedha. Imedaiwa katika kudaiana kulitokea mabishano baina ya wawili hao na wakati Mahimbo akiendelea na shughuli zake, Seif alimvamia na kumpiga na fimbo sehemu ya kichwa na kuanguka.

Majirani walioshuhudia tukio hilo, walipiga kelele kuomba msaada na watu walifika kutoa huduma ya kwanza kabla ya kumpeleka hospitalini.

"Tulisikia kelele ya kuomba msaada, tulipofika Mahimbo alikuwa amelala chini akivuja damu sehemu ya kichwani, tukaanza kumsaidia kupunguza kasi ya uvujaji wa damu na kumkimbiza hospitalini," alieleza mkazi mmoja ambaye hakutaka kuandikwa jina gazetini kwa madai kuwa siyo msemaji.

Nipashe lilimtafuta Kamanda wa Polisi Mkoa wa Tanga, Blasius Chatanda, kuzungumzia tukio hilo na kukiri kulipata na kwamba anasubiri taarifa kamili kutoka kwa maofisa wake ambao wameenda eneo la tukio.

Kamanda Chatanda alisema: "Ngoja tunaendelea na taarifa kwa muda huu na mimi nitazungumza nikishapata taarifa kamili."

HABARI KITAIFA

# Vijiji Muheza vyaanza kusambaziwa umeme

**Na Steven William,** MUHEZA

VIJIJI 13 wilayani Muheza vimesambaziwa huduma ya nishati ya umeme na Shirika la Umeme Nchini (TANESCO), ikiwa ni mpango wa serikali wa kila kijiji na vitongoji vinakuwa na nishati hiyo.

Meneja wa TANESCO wilayani hapo, Chuwa Mathias, aliiambia Nipashe kuwa shirika hilo limeshasambaza huduma hiyo katika vijiji 13 na linaendelea ili kuhakikisha vijiji vyote na vitongoji katika wilaya hiyo vinapata nishati hiyo. Pia, alisema kwa sasa wamesambaza umeme katika vijiji 13 na kuvitaja kuwa ni Kigongomawe, Kilapura, Ngomeni Moja, Masimbani, Ngarani, Kwegole, Kwamkabara na Tingeni. Alivitaja vijiji vingine vinavyofikiwa na umeme huo kuwa ni Lusanga, hospitali mpya ya wilaya, Kwabada na Mafere ambapo na mwezi Aprili, mwaka huu, vijiji vyote vitakuwa vimewaka umeme.

Alisema lengo la serikali ni kuhakikisha vijiji na vitongoji vyote nchini vinawaka umeme ili kuleta maendeleo kwa wananchi kujipatia kipato.

Chuwa alisema mafundi wamesambaa sehemu ya kazi vijijini kujenga laini ndogo za mitaani na kubwa za umeme wenye nguvu ya msongo wa 33 KV na tayari transifoma zimewasili. Kwa upande wake Mhandisi wa kampuni ya RADI ambayo imepewa tenda ya kusambaza umeme wa REA Vijijini, Peter Komele, alisema katika Wilaya ya Muheza wameshasambaza umeme wa REA vijijini asilimia 99.

Alisema walichelewa kumaliza kazi hiyo kutokana na tatizo la mvua.

Meneja wa TANESCO Mkoa wa Tanga, Julius Sabu, alisema mkoa huo umejipanga kuhakikisha vijiji vilivyopangiwa kusambaziwa umeme vinapata vyote.



Waziri wa Maliasili na Utalii, Dk. Damas Ndumbaro, akipata maelezo kutoka kwa Kamishna Uhifadhi wa Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS) kabla ya kuzindua nyumba ya Mhifadhi Mkuu wa Shamba la Miti la Kupandwa la Wino lenye ukubwa wa hekta 39,496.6 linalotoa ajira za muda kwa wakazi wa Halmashauri ya Madaba wapatao 40,000 kila mwaka. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# TASAF yajivunia kubadili maisha

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

MPANGO wa kunusuru kaya maskini, umewezesha wanufaika kubadilisha hali zao za maisha kutoka kuwa vibarua hadi kujiajiri.

Mkurugenzi Mtendaji wa Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF), Ladislaus Mwamanga, alisema hayo wakati akielezea matokeo ya tathmini ya kati ya utekelezaji wa mkakati wa kunusuru kaya maskini awamu ya tatu kipindi cha kwanza.

Alisema tathmini ilibaini kuwa wanufaika wamebadilisha kazi kutoka kuwa vibarua ili kujikimu na kufikia hatua ya kujiajiri wenyewe kwenye kazi binafsi.

Aliongeza kuwa mpango huo umechangia kupunguza kiwango cha umaskini uliokithiri nchini katika familia kati ya asilimia saba hadi 10.

Mwamanga alisema pia walengwa wa mpango waliongeza uandikishaji katika Mfuko wa Afya ya Jamii (CHF), kwa asilimia 21.5 na kuboresha upatikanaji wa huduma za afya kwa familia zao.

Pia, alisema mpango huo umeziwezesha kaya maskini kuzalisha mali na kuwa na uwezo wa kukabiliana na majanga mbalimbali yanayojitokeza kama njaa na ukame.

Alisema kaya nyingi zimeshiriki katika shughuli za uzalishaji mali na kuongeza matumizi ya pembejeo za kilimo na kuzalisha kwa tija ikilinganishwa na ilivyokuwa awali.

"Kwa kutumia ruzuku na ujira walioupata kutokana na mpango walengwa wameboresha maisha yao kwa kuanzisha shughuli za kujipatia kipato na kuwekeza katika maeneo mbalimbali," alisema Mwamanga.

Akizungumzia maeneo ambayo walengwa wamewekeza alisema kaya 27,175 zinafuga ng'ombe 51,299 wakati nyingine 150,043 zinafuga na kumiliki mbuzi 2,745,000.

Alisema katika eneo hilo la ufugaji kaya 38,431 zinafuga na kumiliki nguruwe 781,400 huku kondoo 193,608 wakifugwa na kumilikiwa na kaya 40,066.

Aliongeza kuwa wanakaya wengine 562,934 wamejikita kwenye miradi ya kilimo.

Kwa upande wa uvuvi zipo kaya 33,613 huku nyingine 210,755 zimeanzisha biashara ndogo ili kuongeza kipato na nyingine 183,239 zimeboresha makazi kwa kujenga upya au kukarabati nyumba zao.

Alisema kaya 172,738 zilinunua mabati 1,802,285 ili kuezeka nyumba zao walizokuwa wanajenga na kwamba ni mafanikio ya kujivunia.

# Aipa SUMA-JKT siku 60 kukamilisha tangi la maji

**Na Mwandishi Wetu**

NAIBU Katibu Mkuu Wizara ya Maji, Mhandisi Nadhifa Kemikimba, ametoa siku 60 kwa mkandarasi SUMA-JKT kukamilisha ujenzi wa tangi la maji la Buigiri – Chamwino.

Ujenzi wa tangi hilo utagharimu Sh. milioni 998, kwamba linatarajiwa kuhudumia wakazi wa Chamwino na Hospitali ya Rufani ya Uhuru, jijini Dodoma.

Kwa mujibu taarifa iliyotolewa jana na Kitengo cha Mawasiliano serikalini Mhandisi Kemikimba alitoa agizo hilo wakati alipofanya ziara ya kikazi ya kukagua maendeleo ya ujenzi wa tangi hilo litakalokuwa na ujazo wa lita milioni 2.5.

"Tumekubaliana na mkandarasi kuwa tangi hili likamilike ndani ya mwezi wa pili, kwa hiyo wana siku 60 tu kuhakikisha ujenzi umekamilika," alisema Mhandisi Kemikimba.

Alisema lilipaswa kujengwa tangu Septemba mwaka jana, lakini kutokana na mipango yao imesababisha kuchelewa.

Aidha, ameitaka menejimenti ya Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA), kufanya ufuatiliaji wa ujenzi wa tangi hilo kila siku ili kuhakikisha mradi huo unakamilika kwa wakati.

Katika hatua nyingine, Naibu Katibu Mkuu, Kemikimba alitembelea eneo la Ihumwa panapochimbwa visima na kuagiza kitengo cha uchimbaji kilicho chini ya RUWASA kuongeza kasi ya uchimbaji visima ili kukamilisha miradi kwa wakati.


## TAARIFA KWA UMMA



**BW. ENOSI MWAKAPONDA BUKUKU** ambaye picha yake inaonekana hapo juu, siyo Wakala tena wa Kampuni yetu ya **ZANA BORA LIMITED** kuanzia sasa na mtu yeyote asijihusishe kufanya naye Biashara kwa kuhusisha Kampuni yetu kwa namna yeyote ile.

**UNHCR**
United Nations High Commissioner for Refugees
Haut Commissariat des Nations Unies pour les réfugiés

**REQUEST FOR PROPOSAL: No. RFP/2020/SUP/049**
**FOR THE PROVISION OF INTERNET SERVICES FOR UNHCR TANZANIA OPERATION**

1. **Background:**

The Office of the United Nations High Commissioner for Refugees (UNHCR), Representation Office in Dar es Salaam invites reputable and qualified suppliers to submit firm offers for establishment of the service contract(s) for provision of internet services for UNHCR Tanzania operation.

2. **Eligibility:**

Suppliers duly registered with relevant government authorities, with sound financial basis, relevant experience, reputed clientele and with knowledge of how to meet UNHCR's requirements are invited to participate in the bidding process.

**Kindly download the tender documents in the below link:**

**https://drive.google.com/drive/folders/1fmqQdz_M-FKhM8yZK-MA0qex5mU6rMf_V?usp=sharing**

If you fail to access the link, please write to **ishobeza@unhcr.org** copy **ndassa@unhcr.org**

**CRUCIAL DATES FOR THIS REQUEST FOR PROPOSAL**

| | |
|---|---|
| Pre-bid Conference meeting will be held | Wednesday 06th January 2021 |
| Deadline for receiving requests for clarification | Wednesday 20th January 2021 at 1700 hrs EAT |
| Deadline for submission of offers | Friday 29th January 2021 at 1700 hrs, EAT |

*UNHCR tenders are free of charge, no fees are charged to collect the tenders.*

# NIT yazindua kozi uendeshaji magari viwanja vya ndege

**Na Gwamaka Alipipi**

KATIKA kuboresha sekta ya anga nchini, Chuo cha Taifa cha Usafirishaji (NIT), kimezindua mtaala wa kozi ya utoaji wa huduma za uendeshaji magari ndani ya viwanja vya ndege.

Akizungumza wakati wa uzinduzi wa mtaala huo jijini Dar es Salaam kwa niaba ya Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Viwanja vya Ndege (TCAA), Meneja wa Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere (JNIA), Paulo Rwegasha, alisema hatua hiyo itaongeza ufanisi wa utoaji huduma katika viwanja vya ndege nchini.

Rwegasha alibainisha kuwa kwa kipindi kirefu sekta ya anga nchini imekuwa katika matatizo mbalimbali ikiwamo upungufu wa wataalamu na kukwamisha jitihada za nchi kufikia malengo ya kujiletea maendeleo.

Alisema NIT kutoa mafunzo hayo ni hatua kubwa kwa taifa hususani kipindi hiki ambacho serikali imeonyesha mwanga mkubwa katika kuiinua sekta ya anga hapa nchini.

"Niwapongeze NIT kwa ubunifu huu wa uzinduzi wa kozi ya umahiri wa utoaji ya huduma katika viwanja vya ndege, hii ni hatua kubwa inayopaswa kupongezwa kwa kuwa inazidi kuinyanyua sekta ya anga hapa nchini," alisema Rwegasha.

Alisema ukwasi wa wataalamu hao na marubani kwa kipindi kirefu ni kikwazo kwa taifa kufikia malengo yake jambo lililosababisha kuajiri kutoka nchi zingine na kujikuta ikiingia gharama kubwa.

Aliitaka NIT kuendelea kuwa mfano dhidi ya nchi zingine za Afrika Mashariki kwa kutoa huduma bora, kujikita kwenye kutoa kozi nyingi ili kutoa wataalam watakaosaidia maendeleo ya sekta hiyo nchini.

Kwa upande wake Mkuu wa Chuo hicho, Profesa Zacharia Mganilwa, alisema kuzinduliwa kwa mtaala huo ni mwendelezo wa jitihada za NIT katika kufanikisha malengo maalumu ya utekelezaji wa mipango ya chuo hicho kuiinua sekta ya usafirishaji.

Profesa Mganilwa alisema: "Tunaamini kuwa huu ni mwanzo kwani bado kuna taaluma mbalimbali katika sekta hii. Nasi kama chuo tutaendelea kufungua njia mbalimbali katika ufundishaji."

Alisema katika kulifanikisha hilo NIT imeendelea kuwajengea uwezo wa kitaalamu watumishi wake ambao ndiyo wakufunzi wa masomo hayo na mengine yatakayotolewa na chuo hicho.

Pia, Profesa Mganilwa alisema NIT imeendelea na utoaji wa masomo ya uhandisi wa ndege katika ngazi ya stashahada na kubainisha kuwa matarajio ni baada ya miaka mitano ijayo Tanzania iwe na wahandisi wa fani hiyo zaidi ya 400.

Alisema kutokana na ujenzi wa karakana za utengenezaji wa ndege zinazoendelea kujengwa katika viwanja mbalimbali vya ndege nchini, wahandisi hao watakuwa katika nafasi nzuri katika kutekeleza majukumu yao ipasavyo.




Naibu Waziri wa Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angeline Mabula, akizungumza wakati wa kukabidhi vifaa vya upimaji vya RTK kwa Halmashauri ya Mkuranga akiwa katika ziara ya kikazi mkoani Pwani mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Diwani avalia njuga utengenezaji madawati

**Na Steven William,** PANGANI

JUMLA ya madawati 186 yanahitajika katika Shule ya Sekondari ya Funguni, wilayani Pangani, mkoani Tanga kwa ajili ya wanafunzi wanaoanza kidato cha kwanza.

Diwani wa Kata ya Pangani Magharibi, Ramadhani Saburi, aliwaambia waandishi wa habari wakati akizungumzia maandalizi ya wanafunzi wa kidato cha kwanza katika shule hiyo.

Alisema wanaendelea kujadili masuala ya elimu katika vikao vinavyofanyika katika shule hiyo kwa kushirikiana na bodi ya shule na kupanga mikakati ya kutengeneza madawati hayo.

Diwani huyo alisema kuwa wanafunzi 309 wamefaulu kuanza kidato cha kwanza katika shule hiyo na lengo ni kuhakikisha hakuna mwanafunzi atakayekosa dawati.

Saburi alisema kuwa ili kutatua tatizo hilo kwa haraka madiwani wa kata tatu za mjini Pangani, Bweni, Pangani Mashariki na Pangani Magharibi watatoa madawati 62 na meza.

Saburi alisema anajitahidi kutafuta wafadhili na wadau kusaidia suala la madawati ili kutatua tatizo hilo.

Pia, alisema wanapambana na ujenzi wa vyoo vya wanafunzi na uzio ili kusaidia ulinzi kwa wanafunzi wa bweni kutokana na kuwa mbali na vyoo hivyo.

Kadhalika, aliwataka wananchi na viongozi kutoa kipaumbele kwenye suala la elimu.

# Viongozi watakiwa kumtanguliza Mungu pekee

**Na Ambrose Wantaigwa,** MARA

MAMIA ya waumini wa Kanisa la Tanzania Missionaries Revival Church mjini Musoma, mkoani Mara wameendesha maombi maalum ya kuliombea taifa na kuwataka viongozi wa ngazi zote nchini kumwogopa Mungu.

Akiendesha ibada hiyo mwishoni mwa wiki, Askofu wa kanisa hilo, Jacob Lutubija, alisema viongozi wanaomtanguliza Mungu pekee ndiyo wanaoweza kunusuru taifa na majanga ya kibinadamu ikiwamo magonjwa na ufisadi.

Alisema katika siku za karibuni dunia imekumbwa na ugonjwa hatari wa corona na Rais John Magufuli aliagiza viongozi wa madhehebu mbalimbali na wananchi kusali hatua iliyosaidia kunusuru taifa na maafa.

"Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. John Magufuli, alituonyesha mfano kwa kutukumbusha kama taifa umuhimu wa kumtegemea Mwenyezi Mungu katika kukabili majanga mbalimbali ikiwamo corona na kufanikiwa kushinda," alisema.

Alisema dunia inakabiliwa na kuongezeka matukio ya uharibifu kama vile vita na kuongezeka hofu kutokana na kuwapo mataifa mbalimbali yanayokuwa na viongozi wasiokuwa na hofu ya Mungu.

Mmoja wa waumini kanisa hilo, Rebbeca Nyanjira, alisema wameweka utaratibu wa kuhudhuria misa maalum kila mwezi kwa ajili ya kushiriki kuliombea taifa na kutambua umuhimu wa kuimarisha amani na matendo mema.

"Tukishiriki ibada na kuliombea taifa tunapata faraja ya kuepuka kutenda maovu na kuimarisha amani miongoni mwetu na pia katika jamii inayotuzunguka na taifa kwa ujumla," alisema.

# Kamishna Skauti afanya ziara ujirani mwema

**Na Dotto Mwaibale,**
MBEYA

KAMISHNA Mkuu Msaidizi wa Skauti Tanzania anayeshughulikia makambi na mazingira ambaye ni mlezi wa mikoa ya Mbeya, Ruvuma na Iringa, Mary Anyitike, amefanya ziara ya ujirani mwema mkoani hapa.

Akizungumza na waandishi wa habari mkoani hapa mwishoni mwa wiki, Anyitike alisema lengo la ziara hiyo ni kuangalia utendaji kazi na kutembelea uwanja wa Skauti wa Ali Hassan Mwinyi, mkoani humo.

"Lengo la ziara hii ya siku moja ilikuwa ni kuangalia utendaji kazi na kutembelea uwanja wetu, ambapo pia nilipata nafasi ya kuzungumza na baadhi ya wajumbe wa bodi ya skauti mkoani hapa na kuhudhuriwa na Mwenyekiti wa Bodi wa Skauti, Dk. Julius Kaijage," alisema Anyitike.

Anyitike alisema katika ziara hiyo alizungumza na wananchi wanaoishi jirani na uwanja huo na wafanyabiashara ndogo ndogo kujua matatizo wanayokabiliana nayo ili kupata ufumbuzi na kudumisha ujirani mwema.

Kamishna wa Skauti Mkoa wa Mbeya, Sadock Ntole, alisema ziara hiyo ya kikazi ya Anyitike imewapa mori zaidi wa kazi na kuwa ujumbe walioupata ataufikisha katika wilaya zote za mkoa huo.

"Tumefarijika sana na ziara ya mlezi wetu na yote aliyotuelekeza tutayafanyia kazi," alisema Ntole.



Watalii pamoja na wananchi wakiangalia samaki wawili aina ya jodari wakiwa na uzito wa kilo 75 kila mmoja waliovuliwa eneo la Bahari Kuu Zanzibar, baada ya kufikishwa Shangani jana. **PICHA: MARTIN KABEMBA**

# Biteko aipa jukumu Tume Madini kupitia mikataba

**Na Alphonce Kabilondo,**
GEITA

WAZIRI wa Madini, Dotto Biteko, ameiagiza Tume ya Madini kupitia mikataba waliyoingia na Shirika la Utafiti wa Madini la Serikali (STAMICO) na Kampuni ya TANZAM, katika mgodi wa Bukreefu, Kijiji cha Mnekezi wilayani Geita.

Alitoa agizo hilo alipotembelea mgodi huo na kuona hatua ya ujenzi na kuzungumza na uongozi wa mgodi huo.

Biteko alisema mgodi huo umekuwa na matatizo lukuki na kuiagiza Tume ya Madini kupitia mikataba hiyo, kuirekebisha kama itakuwa na kasoro.

"Tume ya Madini hakikisheni mnapitia mikataba hiyo kama kuna kasoro na kuirekebisha, nataka nikirudi hapa wakati wa Bunge la Bajeti mgodi uwe umeanza kazi ya uzalishaji wa madini," alisema Waziri Biteko.

Mwakilishi wa Kampuni ya TANZAM, Khalaf Rashid, aliahidi kutekeleza agizo lililotolewa na serikali ili kuhakikisha jamii na Watanzania wananufaika na rasilimali zao.

Naye Mhandisi wa mgodi huo, Gaston Mujwahuzi, alisema mgodi huo utakuwa na mitambo miwili, mmoja utakuwa na uwezo wa kuchakata tani 40 za mchanga wa dhahabu kwa saa moja na wa pili utakuwa na uwezo kuchakata tani 220.

Uzalishaji wa mgodi huo utakapoanza Shirika la utafiti la serikali STAMICO litapata mgawo wa asilimia 45 na kampuni ya TANZAM asilimia 55.

Wakati huohuo, Waziri Biteko akiwa katika mgodi wa wachimbaji wadogo wa madini ya dhahabu Kata ya Nyarugusu, aliwaagiza mialo ya uchenjuaji ya michanga ya dhahabu kusajiliwa, ili kudhibiti mianya ya utoroshaji madini ya dhahabu inayo kamatishwa kwa kutumia kemikali aina ya zebaki.

Awali, Ofisa Madini Mkoa wa Geita, Mhandisi Daniel Mapunda, akitoa taarifa fupi alisema Mkoa wa Geita una leseni za uchimbaji wa madini zaidi ya 1,500, leseni 600 zipo katika Wilaya ya Geita na mialo ya uchenjuaji zaidi ya 800.

# Mabula aridhishwa ununuzi vifaa upimaji ardhi

**Na Munir Shemweta,**
PWANI

NAIBU Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angeline Mabula, amezipongeza halmashauri za wilaya ya Mkuranga kwa kununua vifaa vya upimaji.

Akiwa kwenye ziara ya kukagua utendaji kazi wa sekta ya ardhi, Dk. Mabula alisema uamuzi wa halmashauri kununua vifaa huku zingine zikitenga fedha kwa ajili ya mpango kabambe, unaonyesha wakurugenzi wako makini. Dk. Mabula pia alizungumza na watendaji wa sekta ya ardhi, viongozi wa Mkoa wa Pwani na wakurugenzi wa halmashauri za mkoa huo.

Akielezea uamuzi wa kununua vifaa vya upimaji katika Halmashauri ya Mkuranga Mkoa wa Pwani, Dk. Mabula alisema ni jukumu la halmashauri kuihudumia idara ya ardhi ili iweze kufanya kazi vizuri na kwa ufanisi.

Alisema, halmashauri ikinunua vifaa kwa ajili ya idara ya ardhi itaiwezesha idara hiyo kupima maeneo mengi na kuifanya kuwa na maeneo mengi yaliyopimwa na kupangwa na kuepusha migogoro ya ardhi.

"Ukiwa na kifaa chako cha upimaji cha RTK biashara yako ya upimaji katika halmashauri yako ni kazi rahisi sana, unaweza kupima wilaya yako na kuondokana na migogoro ya ardhi," alisema Dk. Mabula.

Aliitaka Halmashauri ya Mkuranga kuhakikisha kifaa ilichokabidhiwa kinatumiwa badala ya kukihifadhi.

Alisema wakati halmashauri nyingine katika mkoa huo zenye uhitaji wa kukitumia zitakapohitaji ziazimwe, ili kuongeza kasi ya upimaji katika Mkoa wa Pwani. Wakati huohuo, Dk. Mabula aliipongeza Halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo kwa uamuzi wa kutenga Sh. milioni 230 kwa ajili ya kuandaliwa mpango kabambe wa Mji wa Bagamoyo.

Alisema, pia imefanya vizuri katika ukusanyaji mapato yatokanayo na kodi ya pango la ardhi.

Dk. Mabula alisema hadi kufikia Desemba mwaka jana imefikia asilimia 54 ya makusanyo yake.


Nestlé Good food, Good life

## TANGAZO LA UWAKALA

Kampuni ya Nestle, office ya Tanzania, inatafuta mawakala wa kusambaza bidhaa zake kwenye kanda na mikoa ifuatayo

- Kanda ya Kaskazini (Tanga, Kilimanjaro, Arusha na Manyara)
- Kanda ya Kati (Morogoro, Dodoma na Singida)
- Nyanda za juu Kusini (Iringa, Mbeya, Songwe, Rukwa na Katavi)

Tanahitaji wakala mwenye maono marefu ya kibiashara na kiu ya kukua na mwenye uwezo wa kukuza bidhaa zetu kupitia usambazaji wa rejareja na ukuaji wa wateja.Kampuni inaahidi mapato mazuri kwa wafanyabiashara watakaoshinda zabuni.

**Vigezo vinavyotakiwa kwa mawakala ni kama vifuatavyo:**

1. Uelewa mkubwa wa eneo husika, njia za mauzo, wateja na uwezo wa kujua makadirio ya mauzo kwa mwezi,nusu mwaka hadi mwaka mzima.
2. Dhamana ya benki ya shilingi milioni 300 za kitanzania toka kwenye benki maarufu hapa nchini
3. Mtaji usiopungua shilingi milioni 500 za kitanzania
4. Ofisi iliyounganishwa mtandao wa intaneti.
5. Ghala lenye nafasi ya kutosha angalau mita mraba 2000(sq)
6. Wauzaji mahiri wa bidhaa angalau 2 kwa ajili ya uchukuaji oda za wateja, 2 kwa kutumia magari na mtunza kumbukumbu mmoja.
7. Awe na uwezo wa kuwa na magari yafuatayo: Canter 2 (tani3) za kuuza mkoa kwa mkoa na magari madogo (Suzuki carry) angalau moja kwa kila mkoa uliotajwa hapo juu.
8. Awe na kampuni iliyosajiliwa Tanzania yenye rekodi nzuri ya ulipaji kodi pamoja na nakala za miaka mitatu za barua za ulipaji kodi (Tax clearance certificates)
9. Kampuni inayojishughulisha na usambazaji au yenye uzoefu na biashara za usambazaji bidhaa itakuwa kwenye nafasi nzuri ya kufikiriwa.

Maombi yepelekwe kwenye anuani ifuatayo kabla ya **tarehe 15 Januari 2021** yakielezea eneo husika la uwakala.

**Meneja maendeleo ya biashara**
**Nestle Tanzania**
**S.L.P. 105665**
**Dar es Salaam**
**Tanzania.**

# MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

## Simba amkeni, kupindua matokeo inawezekana

**WAWAKILISHI** wa Tanzania kwenye michuano ya kimataifa, Simba na Namungo keshokutwa watashuka dimbani katika viwanja tofauti ndani na nje ya nchi kurusha karata zao za mwisho kwenye mechi za marudiano za raundi ya kwanza ya michuano ya Ligi ya Mabingwa na Kombe la Shirikisho barani Afrika. Katika michuano hiyo inayoandaliwa na Shirikisho la Soka Afrika (Caf), Simba inayoiwakilisha Tanzania kwenye Ligi ya Mabingwa Afrika, itaikaribisha FC Platinum ya Zimbabwe katika Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam baada ya mechi ya awali kukubali kipigo cha bao 1-0 ugenini.

Kipigo hicho kwa Simba kimekuja ikitoka kuitoa Plateau United ya Nigeria kwa bao 1-0, lakini kwa upande wa Namungo FC inayopeperusha bendera ya Tanzania kwenye Kombe la Shirikisho Afrika, yenyewe itakuwa nchini Sudan kurudiana na Al Hilal Obayed baada ya mchezo wa kwanza katika Uwanja wa Azam Complex, Chamazi jijini Dar es Salaam, kushinda 2-0.

Hata hivyo, licha ya Simba kuwa nyuma kwa bao 1-0 dhidi ya FC Platinum huku Namungo ikitangulia kwa mabao 2-0 dhidi ya Wasudan hao, hiyo haitoshi kujiamini kwa namna yoyote ile, na badala yake inatakiwa kuhakikisha inaulinda ushindi huo kwa kutafuta bao la mapema ugenini ili kuwaweka wapinzani wao katika presha ya kimchezo. Lakini kwa Simba, hatuoni sababu kushindwa kuibuka na ushindi nyumbani, kwani kama wapinzani wao wameweza wakiwa kwao, kwa nini nayo isitumie vema nafasi hiyo ya kucheza nyumbani wakiwa mbele ya mashabiki wao? Pia tunaamini maandalizi waliyoyafanya kuelekea mchezo huo ni moja ya sababu ya kufanya vizuri ila haina budi kuheshimu wapinzani wao kwani wanaonekana kuwa fiti kimchezo kuliko Plateau United.

Ni wazi wapinzani wao watashuka uwanjani Jumatano wakiwa na lengo moja tu la kupata bao la mapema ili kuwachanganya, hivyo ni vema Simba ikacheza kufa kupona kama fainali mwanzo mwisho huku wachezaji wakiepuka kucheza na jukwaa kwa pasi zao za kisigino na mbwembwe nyingi zisizo na mafufaa kwa timu. Ikumbukwe kwamba hii ni hatua muhimu kwa Simba na Namungo katika kujenga heshima ya soka letu kimataifa, hivyo tunatamani kuona wawakilishi wetu hao wakivuka hatua hiyo na kufika mbali zaidi ili Watanzania waendelee kufurahia burudani ya soka inayoongozwa kupendwa hapa nchini. Tunatambua kama Simba itapata matokeo mazuri ya jumla itatinga moja kwa moja hatua ya makundi na kuwa na uhakika wa kutia kibindoni takriban Sh. bilioni 1.2 kutoka Caf kwa kufika hatua hiyo, lakini, endapo itashindwa kusonga mbele itaangukia Kombe la Shirikisho na kucheza mechi ya mchujo nyumbani na ugenini kusaka nafasi ya kucheza hatua ya makundi ya michuano hiyo.

Hivyo, Nipashe tunatamani kuona Simba ikiendelea kupeperusha bendera ya nchi kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa ambayo inaongoza kwa utajiri kwa ngazi ya klabu Afrika, lakini pia Namungo nayo ikivuka hatua hiyo na ile ya mchujo ili kucheza hatua ya makundi, hilo litawezekana endapo kila mmoja atatimiza wajibu wake kuanzia wachezaji, makocha, viongozi na hata mashabiki. Aidha, ikumbukwe kama Simba na Namungo zitafanikiwa kusonga mbele na kutinga hatua ya robo fainali, itaifanya Tanzania kuongezewa timu moja moja kwenye Ligi ya Mabingwa na Kombe la Shirikisho, hivyo kupeleka jumla ya timu nne msimu ujao, jambo ambalo tunataka kuona likitokea. Kwa mantiki hiyo, mashabiki, wapenzi wa soka na Watanzania kwa ujumla, tuweke ushabiki na mapenzi yetu kando twende kuisapoti mwanzo mwisho Simba ambayo itakuwa nyumbani, tukiwa na lengo la kuiombea pamoja na Namungo ili zifike hatua hiyo muhimu kwa mafufaa ya soka la Tanzania. Nipashe kama mdau namba moja wa michezo nchi, tunazitakia Kila la Kheri Simba na Namungo Kimataifa.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






Na Adam Fungamwango

## Muungwana Lazima Nilonge

### Wanasimba wanataka ushindi na si pasi nyingi

**UKIWA** mtanange wa machozi, jasho na damu keshokutwa, Jumatano wakati wawakilishi wa Tanzania kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika, Simba watakapomenyana na FC Platinum ya Zimbabwe kwenye mechi ya marudiano itakayoamua nani atatinga hatua ya makundi.

Kwenye mechi iliyochezwa wiki mbili zilizopita, Simba ilichapwa bao 1-0, hivyo inahitaji ushindi wa kuanzia mabao 2-0 ili iweze kusonga mbele, vinginevyo itatupwa kucheza mechi ya mchujo ili kutinga hatua ya makundi ya Kombe la Shirikisho Afrika.

Ni pambano gumu ambalo linatakiwa wachezaji wa Simba kujitoa kwa asilimia 100 ili kusaka ushindi mnono.

Simba ina historia ya kutofungwa kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa kwa muda mrefu ikiwa katika mechi za michuano hiyo, lakini pamoja na rekodi hiyo, inaweza isipoteze lakini ikang'oka kama ikitoka sare au ikishinda 2-1.

Najua viongozi, wanachama na mashabiki wa Simba kila moja atakuwa amefanya kazi yake vema. Kazi sasa itakuwa imebaki kwa wachezaji. Wao ndio watakaobeba si bendera ya Simba pekee, bali ya Tanzania.

Kwa jinsi nilivyoiangalia mechi iliyopita ni kwamba Simba bado ilikuwa na hazina ya kuwa na wachezaji wazuri mmoja mmoja kuliko FC Platinum.

Hata hivyo, wachezaji wa Platinum kilichowasaidia walionekana kucheza na kujituma zaidi kuliko wa Simba.

Walikimbia zaidi kuliko wachezaji wa Simba ambao walikuwa wakicheza taratibu wakitegemea ufundi waliokuwa nao miguuni. Wachezaji wa Simba walionekana kucheza wakidhani muda wowote ule wanaweza kupata bao, wakiiangalia timu hiyo kuwa ni ya kawaida sana na isiyo na jina kubwa.

Kwenye mechi ya Jumatano, wachezaji wa Simba wanatakiwa kucheza kwa nia moja tu, nayo ni kusaka ushindi. Ushindi unatakiwa upatikane kwa kucheza soka la moja kwa moja na si tena pasi nyingi na visigino visivyo na sababu.

Simfundishi kazi kocha na wala sisemi kuwa wachezaji wasipasiane bali wawe wanapiga mpira mbele, la hasha kuwahi kutafuta mabao ya mapema. lakini pia ninachosema hapa ni kwamba wachezaji wapunguze pasi nyingi za hapo kwa hapo ambazo hazina sababu yoyote, badala yake pasi yoyote itakayopigwa iwe na sababu ya kutaka kuzaa bao na si vinginevyo.

Kinachotakiwa ni kucheza soka la kushambulia muda wote, huku pia wachezaji wakipunguza kupasiana pasi nyingi ndani za nyuma katika eneo lao la hatari, badala yake mashuti pia yanatakiwa nje ya 18.

Simba ina mapungufu kwa wachezaji wake wengi ukiondoa Said Ndemla, Luis Miquissone na Meddie Kagere kupiga mashuti. Kama kila mchezaji atakuwa na jukumu la kulazimisha kuingia kwenye eneo la hatari na kupiga mashuti makali, basi mechi inaweza kuwa nzuri na rahisi kwao lakini furaha kwa Watanzania.

Kingine ni baadhi ya wachezaji kutaka kukaa na mpira kwa muda mrefu pasipo sababu yoyote. Kuna tabia ya baadhi ya wachezaji kutaka kukaa na mpira wakati kuna wenzake wanaomba, lakini anataka kugeuka na kupiga chenga zisizo na sababu na hiyo inasababisha mara nyingi kunyang'anywa na kuleta hatari langoni.

Wakati mwingine Simba huwa inafungwa magoli si kwa sababu ya ubora wa wapinzani, bali ni kwa sababu ya uzembe wa baadhi ya wachezaji kutaka kukaa na mpira, ili kupiga chenga, ashangiliwe na mashabiki.

Inaweza isiwe hatari kwenye mechi za Ligi Kuu, lakini kwenye mechi kubwa kama hizi za Ligi ya Mabingwa ni zaidi ya hatari.

Simba wakumbuke kuwa wanacheza na wachezaji wenye uwezo mkubwa na wazoefu kwenye michuano hii, hivyo wasiwafanye kama wale wanaokutana nao kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara.

Kukiwa na moyo wa kujituma, kila mchezaji akitekeleza majukumu yake na kufuata maelekezo yote, sidhani kama kuna kitu kitashindikana. Platimun si wazuri kama walivyokuwa Nkana FC mwaka 2018.

Walikuja nchini wakiwa mbele kwa mabao 2-1, lakini Simba ilipindua matokeo kwa kushinda 3-1. Na kwa bahati nzuri wachezaji wengi ni walewale, huku wakiwa wameongezeka baadhi wenye uwezo mkubwa. Ni suala ya wachezaji kujituma tu. Inawezekana.

# HABARI PICHANI



Kamishna wa Uhifadhi TFS, Prof. Dos Santos Silayo (aliyeshika mche wa mti), akimdadisi Meneja wa TFS Wilaya ya Mbinga, Kelvin Mpiluka, mwitikio wa wananchi katika kuomba miche ya miti kwa ajili ya kupanda kwenye maeneo yao, katika kipindi hiki cha mvua zinazoendelea. **PICHA: MPIGA PICHA WETU**



Wafanyabiashara wa Soko Kuu la Majengo Jiji la Dodoma wakiuza matunda yao, huku yakiwa yamepangwa chini badala ya mezani bila kujali afya za walaji na wao wenyewe. **PICHA: PETER MKWAVILA**



Mti ukiwa umedondoka na kuziba barabara na kuleta usumbufu kwa waendesha magari na watembea kwa miguu, ulianguka kutokana na mvua kubwa iliyonyesha jana, jirani na jengo la PSSSF na Makao Makuu ya Jeshi la Zimamoto na Uokoaji jijini Dodoma. **PICHA: PETER MKWAVILA**



Mwendesha pikipiki maarufu (bodaboda), akiwa amepakia abiria kinyume na sheria katika eneo la Kitunda Kivule jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**




Askofu wa Kanisa la Power of Good Fire, Dankton Rweikila, akiongoza mahubiri wakati wa ibada ya kuliombea amani Taifa katika kuingia mwaka mpya wa 2021, kanisani hapo, Chanika jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**



Baadhi ya watoto wakisherehekea kuona mwaka mpya wa 2021, Mazubu Grand Hoteli, Mji Mdogo wa Mirerani wilayani Simanjiro, mkoani Manyara, juzi. **PICHA: GIFT THADEY**

# Waziri aagiza TANROAD kupunguza gharama miradi

**Na Gwamaka Alipipi**

WAZIRI wa Ujenzi na Uchukuzi, Dk. Leonard Chamuriho, ameagiza Wakala wa Taifa wa Barabara (TANROAD), Mkoa wa Mara, kupunguza gharama za miradi hususani wanapofanya upembuzi yakinifu.

Alitoa agizo hilo wilayani Bunda, akikagua ujenzi wa barabara ya Nyamuswa, Bunda hadi Kisorya yenye urefu wa kilometa 121.9, pamoja na kipande cha barabara ya lami kutoka Bulamba hadi Kisorya chenye kilometa 51.

Akiwa katika ukaguzi huo, Waziri Chamuriho alisema barabara ya Nansio, ambayo inaanzia Nyamuswa, Bunda hadi Kisorya ni muhimu kwa wananchi wa Bunda na kwamba itafungua fursa nyingi ikiwamo usafirishaji wa mazao.

Mkuu wa Wilaya ya Bunda, Lydia Bupilipili, alimpongeza mkandarasi wa barabara hiyo na TANROADS kwa kazi nzuri waliyoifanya ya kusimamia ujenzi.

Bupilipili alisema: "Kasi ya ujenzi ilikuwa kubwa katika barabara hii na imetoa ajira kwa vijana wazawa wa wa Bunda na mkoa wa Mara. Niwapongeze TANROAD kwa kazi nzuri wanayoifanya katika Wilaya ya Bunda Mjini."

Kwa upende wake Meneja wa TANROAD, Mkoa wa Mara, Mlima Ngaile, akitoa taarifa ya utekelezaji wa mradi huo alisema mkataba ulisainiwa na makubaliano yalikuwa ya miaka miwili, lakini kutokana na kasi ya mkandarasi aliahidi kumaliza kazi hiyo kabla ya muda uliopangwa.

"Thamani ya mkataba Sh. bilioni 46.5 na unasimamiwa na kampuni ya wahandisi ya ushauri wa TANROAD na hadi kufikia sasa mkandarasi ameshaanza kazi mbalimbali ikiwamo kujenga nyumba ya msimamizi ambayo imefikia asilimia 50 na amesafisha barabara kutoka Bunda kwenda Bulamba."



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa (aliyepiga magoti), akipanda mti wa mwembe dodo ulioboreshwa ikiwa ni sehemu ya kumbukumbu ya kuitembelea Shule ya Sekondari ya Wavulana Tunduru na kukagua ukarabati unaoendelea. **PICHA: STEVE CHINDIYE**

# DC ataka udhibiti mabanda ya video

**Na Gurian Adolf,**
SUMBAWANGA

MKUU wa Wilaya ya Sumbawanga mkoani Rukwa, Dk. Halfan Haule, amewaagiza viongozi wa serikali za vijiji na mitaa kuvipiga marufuku vibanda vya kuonyesha picha za video na mpira wa miguu, vinavyochangia kupotosha watoto pamoja na wanafunzi.

Amesema sehemu hizo maarufu kwa jina la vibanda umiza zinawanasa wanafunzi wanaokimbilia burudani mabandani badala ya kujisomea, huku wengine wakitumbukia kwenye uhalifu na mimba utotoni.

Alitoa agizo hilo hivi karibuni wakati akizungumza na wanahabari kuhusu utekelezaji wa mpango mkakati wa kuzuia mimba na ndoa za utotoni wilayani humo.

Awali, mkakati huo ulizinduliwa na serikali ya mkoa huo kwa lengo la kumaliza mimba shuleni na ndoa za mabinti.

Mpango mkakati wa kukabiliana na ndoa pamoja na mimba za utotoni mkoani Rukwa unatekelezwa na mashirika mbalimbali likiwamo la Youth Education Through Sports (YES-Tanzania) kwa ushirikiano na Plan International.

Dk. Haule alisema baadhi ya watu wanaosimamia vibanda hivyo wamekua wakiruhusu watoto pamoja na wanafunzi kwenda kuona video za aina mbalimbali na mpira wakati wanajua kuwa sheria haziruhusu hilo, lakini wamekuwa wakikaidi kwa makusudi.

Mkuu huyo wa wilaya alieleza kuwa baadhi ya wanafunzi hasa wa kike wamekuwa wakikutana na wanaume kwenye vibanda hivyo na kusababisha mienendo mibovu na kupata ujauzito, kisha kukatisha masomo.

Alisema kuwa baadhi ya vibanda hivyo hasa maeneo ya vijijini vimekuwa vikifanya biashara hadi usiku wa manane na mabinti wanafunzi wakiangalia video mbalimbali na kuhatarisha usalama wa maisha na masomo yao.

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Sumbawanga, Nyangi Msemakweli, alisema wamejipanga kuhakikisha ujenzi wa shule za sekondari katika kata 10 za halmashauri ambazo hazina sekondari unafanyika upesi ndani ya mwaka huu.

Alisema lengo ni kuwasaidia wanafunzi wanaotembea umbali mrefu kufuata masomo kwa vile baadhi yao hasa wasichana wanakutana na vishawishi vingi njiani vinavyowasababisha wajiingize kwenye mahusiano na kupata ujauzito katika umri mdogo.

# Katambi atoa maelekezo kukabili uhaba walimu

**Na Marco Maduhu,**
SHINYANGA

WANAFUNZI takribani 1,000 wa Shule ya Msingi Twendepamoja, mkoani Shinyanga wanafundishwa na walimu watano pekee.

Kutokana na upungufu huo, serikali imeiagiza Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga, kupeleka walimu katika shule hiyo iliyoko pembezoni kukabiliana na upungufu huo.

Naibu Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana na Ajira, Patrobasi Katambi, alimwagiza Mkurugenzi wa Halmashauri ya Shinyanga, Geoffrey Mwangulumbi, kupeleka walimu katika shule hiyo iliyoko Mwamalili, kukabiliana na upungufu huo.

Katambi ambaye ni Mbunge wa Shinyanga Mjini, alisema hayo juzi wakati akikagua na kushiriki ujenzi wa vyumba vya madarasa katika shule za msingi na sekondari za Manispaa ya Shinyanga.

Akiwa na wapigakura wake alikutana na matatizo mbalimbali ya shule hiyo ambayo ina walimu watano na mmoja akiwa mbioni kuondoka.

Alisema hajaridhishwa na idadi ya walimu wanaofundisha shule hiyo ya Twendepamoja ambao ni watano tu, ikilinganishwa na wanafunzi 984 wanaowahudumia na kumwagiza mkurugenzi kuchukua hatua.

Alimtaka mkurugenzi wa manispaa kupeleka walimu katika shule hiyo ambayo iko pembezoni mwa mji na kumaliza shida ya ukosefu wa wanafunzi.

"Tatizo hili la upungufu wa walimu katika shule hii ya Twendepamoja limenigusa sana, haiwezekani wanafunzi 984 wafundishwe na walimu watano pekee tena nimepewa taarifa kuwa mwalimu mmoja naye anataka kuondoka, hivyo watabaki wanne, naomba mkurugenzi unasambaza walimu kuwapo na uwiano sawa kwa shule zote," alisema Katambi.

Katika hatua nyingine alieleza kuridhishwa na kasi ya ujenzi wa madarasa kwenye manispaa hiyo, na kupongeza wananchi kushiriki kuchangia ujenzi wake na kutoa Sh. milioni 34 ili kuwaunga mkono, na kuahidi kutafuta wadau ambao watasaidia kununua madawati.

Kwa upande wake Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Shinyanga Mwangulumbi, aliahidi kuzingatia maelekezo hayo na kubainisha kuwa walimu wapya ambao wataajiriwa na kupelekwa kwenye manispaa hiyo, watawapelekwa kwenye shule zilizopo pembezoni ili kumaliza tatizo hilo.

Aidha, Meya wa Manispaa ya Shinyanga David Nkulila, alisema kasi ambayo wemekwenda nayo kwenye ujenzi huo wa madarasa, watakuwa nayo kwenye utekelezaji wa miradi mingine mbalimbali ya maendeleo kwa wananchi.

HABARI KITAIFA

# Waislamu watakiwa kuthamini yatima

**Na Rose Jacob,** MWANZA

BARAZA Kuu la Waislamu Tanzania (BAKWATA), Mkoa wa Mwanza limewataka waumini wa dini hiyo kuutambua mwaka mpya ambao ndio dira katika kutenda mambo ya maendeleo ndani ya jamii.

Akizungumza katika hafla fupi ya chakula cha pamoja na watoto zaidi ya 200 yatima na waishio mazingira magumu, Sheikh Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, Hassan Kabeke, alisema, waislamu wengi wameshindwa kutambua kama kuna mwaka wa Kiislamu na mwaka wa kidunia jambo ambalo sio sahihi. "Mwaka wa Kiislamu unatambulika kidini, kuna mwaka wa kidunia ambao ndiyo umekuwa ukitumika katika mambo muhimu, ikiwamo mwaka wa kuzaliwa, kupata ajira kumbukumbu ya vifo tarehe za ndoa, hivyo sisi Waislamu tunapaswa kuutambua maana huwezi kuandikiwa mwaka wa kidini katika mambo niliyoyataja hapo juu," alisema Kabeke.

Alisema kwa mjibu wa vitabu vya dini kila nyumba ya Mwislamu kunatakiwa kuwamo na mtoto yatima anayelelewa, lakini Waislamu wengi hawatambui wajibu wao.

Naye Mbunge wa Jimbo la Nyamagana, Stansilaus Mabula, aliyekuwa mgeni rasmi katika hafla hiyo, alianzisha mpango wa kuwapatia bima ya afya yenye gharama ya 54,000, watoto yatima ili kuwasaidia katika afya na kwa mwaka 2021 ameanza na watoto 50. "Sisi viongozi na wananchi kwa ujumla tunalo jukumu la kuwalea watoto hawa katika mafundisho ya dini ili wakuwe wakiwa na hofu ya Mungu, huku tukiwajali kiafya ili nao watimize ndoto zao na wenye afya bora, hivyo tutakuwa tumetengeneza taifa zuri la kesho lenye nguvu kazi thabiti," alisema Mabula.

Mkurugenzi wa Jiji Kiomoni Kibamba, pamoja na Katibu wa CCM Mkoa wa Mwanza, Julias Peter na Mkuu wa Wilaya ya Magu, Salum Kali, walisema, serikali imeweka utaratibu mzuri kwa watoto yatima na waishio katika mazingira magumu ni lazima wapate elimu, upendo na wasibaguliwe. "Wajibu wa kulea watoto yatima ni dhamana tuliyopewa na Mungu, wanatakiwa wasomeshwe wasibaguliwe eti wakike au wakiume maana wote wanahaki, hivyo mwaka huu uwe wa amani, upendo, maendeleo na kuliombea taifa pamoja na Rais John Magufuli," walisema.

# Ubovu barabara wakwamisha wananchi vituo vya afya

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

WAKAZI wa kata za Madilu na Milo, wilayani Ludewa mkoani Njombe, wamesema wapo hatarini kupoteza maisha yao kwa sababu ya kushindwa kupata huduma ya afya kwa wakati kutokana na ubovu wa barabara.

Walisema hayo mwishoni mwa wiki baada ya Mbunge wa Jimbo la Ludewa, Joseph Kamonga, kuwatembelea akiwa ameongozana na Meneja wa Wakala wa Barabara Mijini na Vijiji (TARURA), Mkoa wa Njombe, Ibrahim Kibassa, kutokana na malalamiko ya wananchi hao kuhusu ubovu wa barabara.

Walisema kwa muda mrefu barabara ya Madilu kupitia Ilawa, Ilininda kwenda Mundindi, imeharibika na kushindwa kupitika hali inayosababisha wagonjwa kushindwa kupelekwa kwenye vituo vya afya kwa kuwa magari yanashindwa kupita kwenye barabara hizo.

Wakizungumza na Nipashe baadhi ya wakazi hao akiwamo John Mgina, alisema kutokana na ubovu wa barabara hizo kipindi cha mvua wamiliki wa magari wanapandisha nauli kitendo kinachosababisha kushindwa kumudu na wagonjwa kubaki nyumbani bila ya kupatiwa matibabu.

"Kutokana na ubovu wa barabara hasa kipindi cha mvua bei ya nauli hupanda na wakati mwingine magari yanashindwa kufika kabisa maeneo mbalimbali," alisema Mgina.

Mariam Mhagama kwa upande wake alisema, kutengenezwa kwa barabara hiyo kutasaidia wajawazito wanaokuwa katika kipindi cha hatari kupoteza maisha wakichelewa kupata huduma.

"Tunaomba tutengenezewe barabara hii ili kuokoa maisha ya mama majamzito na watoto kwa sababu hatari za barabara kuwa mbovu inaweza kusababisha tukazalia njiani," alisema Mariam.

Mbunge Kamonga alimwomba Meneja wa TARURA, Mkoa wa Njombe kupitia vikundi kwenye kata husika na vijiji vilivyosajiliwa na kutambuliwa na serikali kufanya kazi za ujenzi wa barabara hizo.

Aliiomba serikali kuiwekea bajeti ya kutosha Barabara ya Madilu, ili iweze kupitika muda wote na kufungua sekta nyingine za uchumi.

"Kuna barabara inatoka Madilu kwenda Lugalawa kupitia Mlima Lupungulu inaokoa maisha ya walio wengi wanaokwenda kutibiwa katika Hospitali ya Lugalawa," alisema Kamonga.

Naye Meneja Kibassa, aliahidi kupitia vikundi vilivyopo kata hizo, ujenzi utaanza mara moja katika maeneo korofi ili barabara ziweze kupitika kipindi chote hasa cha mvua.

Alisema katika mwaka wa fedha 2020/2021, serikali imetenga zaidi ya Sh. bilioni nane kwa ajili ya ujenzi wa barabara za wilaya za mkoa huo na kwa Wilaya ya Ludewa imetengwa Sh. bilioni 1.2.

"Tayari mkandarasi ameshapatikana kwa ajili ya ujenzi wa barabara mbalimbali za Ludewa na alitakiwa kuanza kazi kipindi hiki ila kutokana na hali ya mvua inaweza kuharibu zaidi miundombinu hiyo," alisema Kibassa.



Naibu Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana na Ajira, Patrobas Katambi ambaye ni Mbunge wa Jimbo la Shinyanga Mjini (katikati), akishiriki na wananchi ujenzi wa vyumba vya madarasa kwa kusawazisha mchanga, katika shule ya Msingi Mlimani iliyopo Oldshinyanga, jana, **PICHA: MARCO MADUHU**

# Mhashamu Askofu Mkude astaafu rasmi

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

MHASHAMU Askofu Telesphor Mkude wa Jimbo Katoliki la Morogoro, amestaafu rasmi kuliongoza jimbo hilo baada ya Baba Mtakatifu Francisko kuridhia ombi lake la kupumzika katika nafasi hiyo.

Uamuzi huo ulitangazwa usiku wa mkesha wa kuukaribisha mwaka mpya 2021 na Msimamizi wa Kitume wa Jimbo Katoliki la Morogoro, Monsinyo Lazarus Msimbe,kwa mapadre na waumini wa kanisa hilo wakati akiwasilisha salamu zake.

Alisema pamoja na kufikisha salaam za mwaka mpya wapo baadhi ya mapadri, watawa na baadhi ya waamini wananiuliza maswali kwamba Desemba 30, mwaka jana ilitokea taarifa ya kustaafu kwa Mhashamu Askofu Telesphor Mkude; "na mimi nasema ni ya kweli kwani toka lini Vatican wanadanganya, hiyo habari imetoka Vatican ni habari ya kweli.

Alisema kwa kifupi alipata barua ya uteuzi wiki mbili zilizopita kabla ya mwaka mpya kutoka katika Kongagrashio Idara inayoshungulikia uinjilishaji wa watu.

Alisema, barua hiyo ya uteuzi imemtaka aliongoze Jimbo Katoliki Morogoro kama Msimamizi wa Kitume katika jimbo ambalo liko wazi. Vile vile, alisema hapo nyuma alikuwa Msimamizi wa Kitume akiongoza Jimbo Katoliki la Morogoro likiwa na Askofu wa Jimbo kwa lugha ya kilatini.

"Awali mimi nilikuwa Msimamizi wa Kitume wa Jimbo Katoliki la Morogoro lenye askofu, lakini sasa ni Msimamizi wa Kitume wa Jimbo Katoliki ambalo halina askofu kwa maana kwa sasa ninawajibika moja kwa moja kwa Baba Mtakatifu Vatican," alisema.

Tangu Februari 12, 2019, majukumu yote ya katika Jimbo Katoliki, kufundisha, kuongoza na kuwatakatifu watu wa Mungu amekuwa yakisimamiwa na Monsinyo Vitalis Msimbe, ambaye aliteuliwa na Baba Mtakatifu Francisko kuwa Msimamizi wa Kitume wa Jimbo hilo.




Meneja Uhusiano Serikalini Benki ya NMB Kanda ya Kati, Peter Masawe (kushoto), akimkabidhi msaada wa madawati Mkuu wa Mkoa wa Singida, Dk. Rehema Nchimbi (wapili kulia), NMB ilikabidhi madawati 100 kwa ajili ya shule mbili za Wilaya ya Mkalama mkoani humo, yenye thamani ya Sh. milioni 10, Shule ya Msingi Msingi na Ndala. Kulia ni Mkuu wa Wilaya ya Mkalama, Mhandisi Jackson Masaka. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wakulima korosho watahadharishwa dhidi matapeli

**Na Stevie Chindiye,** TUNDURU

WAKULIMA wa korosho wilayani Tunduru mkoani Ruvuma, wametakiwa kuacha kuwatumia watu wasio wafahamu kuwasaidia kutoa fedha zao benki, ili kuepuka kutapelewa na kuibiwa fedha zao.

Rai hiyo imetolewa na Mwenyekiti wa Chama Kikuu cha Ushirika wa Wakulima Tunduru (TAMCU), Hashim Mbalabala, wakati akiongea na wakulima waliokuwa wakiuza kwenye mnada wa 11 wa kuuza korosho uliofanyika katika viwanja vya Chama cha Msingi Mlingoti Mashariki AMCOS.

Akifafanua taarifa hiyo, Mbalabala alisema chama kikuu kina taarifa nyingi za wakulima wake kutapelewa na kuibiwa fedha zao na makundi ya vijana ambao hujifanya wasamaria wema kujitolea kuwasaidia wazee kutoa fedha zao kupitia mitandao ya simu na ATM za benki na baada ya kujua namba za siri huhamisha fedha kwenda kwenye akauni zao au namba za simu na kutokomea.

Alisema ingawa matukio ya wizi yanaonekana kupungua katika msimu huu wa mwaka 2020/2021 ikiwa ni tofauti na msimu wa mwaka 2019/2020, kulikuwa na asilimia 75 ya matukio ya wakulima kutapeliwa na makundi hayo.

Katika mnada huo ambao walijitokeza wanunuzi watano, kati yao mnunuzi mmoja aliomba nunua korosho zote kupitia maombi ya barua na wakulima hao waliuza koshoro zote na za daraja la kwanza ziliuzwa kwa bei ya Sh. 2,100 na daraja la pili kwa Sh. 1,622.

Awali, ofisa ushirika wa Wilaya ya Tunduru, George Bisani, alisema jumla ya kilo 183,328 za daraja la kwanza na kilo 55,659 za korosho daraja la pili zilikwa mtandaoni kwa ajili ya kuwataka wanunuzi kushindania kununua kupitia utaratibu wa kuomba kuzinunua kupitia barua za kutumbukiza kwenye sanduku na mfumo wa mtandao TMX.

Alisema kutokana na mauzo hayo jumla ya Sh. 475,367,698 zilipatikana na zinatarajiwa kuingizwa kwenye akaunti za wakulima baada ya taratibu za malipo kutoka kwa mnunuzi aliyeshinda mnada huo kukamilika.

Meneja Mkuu wa TAMCU, Imanai Kalembo, alisema mwenendo wa malipo unakwenda vizuri na hadi sasa ofisi yake imekwisha idhinisha malipo ya minada 10 kwa vyama vya msingi kwa ajili ya kuwalipa wakulima wao.

# TAMISEMI yatoa mamilioni kukamilisha madarasa

**Na Samson Chacha,** TARIME

HALMASHAURI ya Rorya mkoani Tarime imepata Sh. 246,600,000 kutoka Wizara ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) ili kuongeza juhudi za kukamilisha madarasa 14.

Madarasa hayo ni saba ya shule za msingi, saba ya sekondari na Mkuu wa wilaya hiyo, Simon Odunga, amewahimiza wananchi kuchangia kukamilisha ujenzi wa madarasa hayo ambayo yanatarajiwa kutumika mwezi huu.

Alizitaja shule za msingi zilizopata fedha hizo kuwa ni Nyasoko iliyopata Sh. 46,600,000, Nyanjage (Sh. 44,400,000), Nyamagongo (Sh. 47,700,000), Mori (48,800,000), Sokoraboro (46,600,000), Kuruya (47,700,000) na Mika (47,700,000).

Shule za sekondari zilizopata fedha hizo ni Bukama (40,000,000) kwa madarasa mawili na Sh. 80,000,000 kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa bweni la kidato cha tano na sita na Sh. 6,600,000, ujenzi wa matundu sita ya vyoo.

Shule nyingine ni Ngasaro Sh. 40,000,000, ujenzi wa vyumba viwili vya madarasa, Sh. 40,000,000 kwa Shule ya Adam Malima, vyumba viwili vya madarasa na Sh. 6,000,000 kwa Shule ya Sekondari Kigunga kwa ajili ya kuezeka paa lililoezuliwa na upepo wa mvua.

Odunga aliitaka jamii ya Rorya kuchangia nguvu katika maendeleo ikiwamo ujenzi wa vyumba vya madarasa, ili wanafunzi waweze kusoma katika madarasa bora kwa kuunga mkono juhudi zinazofanywa na serikali.

Pia, aliwataka wazazi wenye wanafunzi waliofaulu kuingia kidato cha kwanza mwaka huu, kuwaandaa watoto wao na kuripoti katika shule zao walizochaguliwa na kwa wale watakaokwamisha wanafunzi kutoripoti shule wazazi hao watachukuliwa hatua kali za kisheria. “Kila mzazi mwenye mwanafunzi aliyefaulu kwenda sekondari ahakikishe mtoto wake anakwenda shule bila kukosa,” alisema Odunga.

## Walimu wazalendo kuboresha elimu

**Na Yamine Protace,** MKURANGA

KIKUNDI cha walimu wazalendo katika Wilaya ya Mkuranga, mkoani Pwani, kimejizatiti kuboresha kiwango cha taaluma kwenye shule za awali na msingi ili kuongeza ufaulu katika shule za sekondari.

Hayo yalisemwa na walimu hao, wakati walipokuwa wakizungumza kwa nyakati tofauti na Nipashe.

Walisema lengo lingine ni kuwaandaa watoto hao waweze kunufaika na ajira zilizopo katika viwanda zaidi ya 80 vilivyopo Mkuranga.

Mwalimu Bakari Jiri, aliye kitengo cha elimu ya msingi katika halmashauri hiyo, alisema uboreshaji wa madarasa unalenga kuondoa kutojua kusoma, kuandika na kuhesabu (KKK).

Mwalimu wa Shule ya Msingi Kiziko Mkuranga, Hadija Embue, alisema michango wanayoitoa katika sekta mbalimbali ni kuonyesha uzalendo wao kwa makundi wakiwamo wagonjwa na watoto wenye uhitaji maalumu.

## Kanisa lafanya maombi ya mwaka mpya

**Na Timothy Itembe,** MARA

KANISA la Roho Kazi ya Messiha limefunga mwaka 2020 na kuukaribisha mwaka mpya 2021 kwa kufanya maombezi ya kuwaponya wagonjwa na kuombea Taifa laTanzania.

Kadinari Joseph Ariyo wa Kanisa la Nyamwaga, wilayani Tarime, alisema wanalazimika kufanya hivyo kutokana na kurudisha shukrani kwa Mungu kuwalinda, kumaliza mwaka 2020 na kumuomba katika utukufu wake kuwasogeza katika mwaka mwingine wa 2021.

Kanisa la Roho Kazi ya Messiha Afrika Mashariki (ukanda wa maziwa makuu), lenye makao makuu mkoani Mara, kijiji cha Ikoma wilayani Rorya, limetumia siku mbili kufanya huduma hiyo, huku likiwataka waumini kuendelea kumtegemea Mwenyezi Mungu katika mambo yote kwa kuwa yeye anaweza badala ya kwenda kuwategemea wanadamu.

Kanisa hilo pia lilimuombea Rais John Magufuli kuendelea kumcha Mungu na taifa lake kwa kumtanguliza katika ugonjwa wa corona na kushinda huku mataifa mengine yakijiuliza Tanzania imeshindaje vita hiyo.

Baraka Biseko mkazi wa Kogaja wilayani hapo alishukuru kwa maombi ya siku mbili yaliyofanyika na kuomba kanisa hilo kuendelea kuendeza Injili ya Bwana.

Nipashe
Spotika




WACHEZAJI 10 BORA WA LIGI KUU UFARANSA 2020 UK. 12-13



# KLABU 5 ZILIZOKATISHA TAMAA MWAKA 2020

**ISIKUPITE**

KATIKA historia ya Ligi Kuu England, mchezaji pekee aliyehusika katika mabao mengi katika mechi zake 30 za mwanzo alizocheza kwenye ligi hiyo zaidi ya Andrew Cole (37 - mabao 28, pasi za mwisho tisa), ni Bruno Fernandes (33 - mabao 19, pasi za mwisho 14).



**LONDON,** England

KILA mwaka unaanza na mipango na malengo kwa taasisi zote, na kwenye klabu za soka hakuna tofauti. Kila msimu unakuja na changamoto zake, huku usajili na kubadilika kwa utawala ni moja ya hatua zinazochukuliwa kwa ajili ya kutimiza malengo.

Kwa kawaida kila klabu inakuwa na malengo tofauti kabisa katika kila msimu. Wakati nyingine zikiwa na malengo ya kupambana kubakia kwenye Ligi Kuu na kuepuka kushuka daraja, zingine zina lengo la kuwa katikati ya msimamo.

Hata hivyo, kwa klabu kubwa kila moja malengo yanakuwa ni kutwaa mataji makubwa katika kila mashindano wanayoingia. Hata hivyo, mwaka 2020 ulikuwa na changamoto nyingi sana, kwani mlipuko wa virusi vya corona ulitikisa kabisa ulimwengu wa soka. Licha ya changamoto hizo, Liverpool walifanikiwa kushinda taji lao la kwanza la Ligi Kuu England kwa mara ya kwanza kwa kipindi cha miaka 30.

Huku wao Bayern Munich wakibeba mataji matatu, likiwamo la Ligi ya Mabingwa Ulaya. Hapa, tunaangalia klabu tano ambazo zilikatisha sana tamaa kwa mwaka 2020.

### #5. BENFICA

Benfica ndio klabu yenye mafanikio makubwa zaidi katika historia ya soka la Ureno na waliingia kwenye msimu wa 2019-20 kama bingwa mtetezi wa Ligi Kuu ya nchini hiyo, maarufu kama Primeira Liga.

Hata hivyo, walishindwa kutetea taji, walimaliza wakipitwa pointi tano nyuma ya Porto waliotwaa ubingwa.

Kumaliza kwao nafasi ya tatu kwenye makundi ya Ligi ya Mabingwa Ulaya mwaka 2019 ikamaanisha kwamba wameshushwa hadi Ligi ya Europa. Hata hivyo, Benfica wakajikuta tena kwenye wakati mgumu, wakafungwa kwa uwiano wa mabao 5-4 na Shakhtar Donestk kwenye raundi ya 32.

Wakashindwa kufuzu kwenye Ligi ya Mabingwa msimu huu baada ya kutolewa na PAOK. Pia wakafungwa kwenye fainali ya Kombe la Ureno, ambapo walichezea kichapo cha mabao 2-1 kutoka kwa Porto na pia wakafungwa kwenye Kombe la Ureno la Super na wapinzani wao hao kwa mabao 2-0, Desemba 2020.

### #4. INTER MILAN

Inter Milan ilituma ujumbe wa mafanikio wakati walipomteua Antonio Conte kuwa kocha wao mkuu wakati wa kipindi cha majira ya joto mwaka 2019.

Kocha huyo wa zamani wa Chelsea alijithibitishia mwenyewe kama mmoja wa makocha bora duniani na alipotua pale San Siro akaungwa mkono kwa usajili wa nyota kadhaa.

Hata hivyo, mwanzo wake na Nerrazurri haukwenda kama ulivyotarajiwa, waliondolewa kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya hatua ya makundi na kutupwa kwenye Ligi ya Europa.

Miamba hao wa Serie A wakapambana na kufika fainali Agosti 2020, lakini wakafungwa mabao 2-1 na Sevilla. Pia Kombe la Coppa Italia wakatolewa na Napoli kwenye nusu fainali na walimaliza nafasi ya pili kwenye msimamo wa Ligi Kuu nyuma ya Juventus.

### #3. MANCHESTER UNITED

Manchester United ilikuwa moja ya klabu iliyokatisha sana tamaa kwa mwaka 2020 na ilikuwa na kiwango kisichovutia kwa mwaka wote.

'Mashetani Wekundu' hao hawakuwa kwenye kiwango chao kilichozoeleka chini ya kocha wao Ole Gunnar Solskjaer.

Walikuwa wakipata matokeo mazuri dhidi ya klabu kubwa kwenye Ligi Kuu England, lakini wakawa wanachezea kichapo mara kwa mara kutoka kwa timu za chini. Mwaka 2020, walifuzu kwenye nusu fainali tatu, lakini waliishia hapo hapo na kushindwa kusonga mbele.

Walitolewa kwenye hatua ya makundi kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya, baada ya ushindi wao wa kwanza katika mechi mbili dhidi ya Paris Saint-Germain na RB Leipzig.

### #2. MANCHESTER CITY

Tofauti na klabu nyingine kwenye orodha hii, Manchester City walimaliza mwaka 2020 wakiwa na taji baada ya kushinda Kombe la Ligi kwenye fainali dhidi ya Aston Villa.

Walipokonywa taji la Ligi Kuu England na Liverpool, huku wakifungwa na Arsenal kwenye nusu fainali ya Kombe la FA.

Na matokeo yaliyowaumiza zaidi kikosi hicho cha Pep Guardiola ni pale walipotolewa kwenye robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya kwa kufungwa 3-1 na Olympique Lyon.

### #1. BARCELONA

Mwaka 2020 kamwe hautasahaulika kwa Barcelona, na pengine ndio klabu iliyokuwa na mwaka mbaya zaidi.

Walianza kwa kufungwa 3-2 na Atletico Madrid kwenye nusu fainali ya Kombe la Hispania, Januari.

Kocha, Ernesto Valverde akafukuzwa na nafasi yake akapewa, Quique Setien. Kocha huyo wa zamani wa Real Betis hakudumu kwa zaidi ya miezi saba katika kazi yake hiyo. Wakati LaLiga ilipoungana na dunia nzima kusimamisha ligi Machi mwaka 2020, Barcelona walikuwa na faida ya pointi mbili kileleni mwa msimamo katika mbio za kuwania taji.

Lakini mwisho wa siku wakajikuta wamepitwa pointi tano na wapinzani wao, Real Madrid ambao walilibeba taji hilo.

Hata hivyo, kipindi kibaya zaidi ni pale walipokumbana na kipigo cha mbwa mwizi, wakati walipofungwa mabao 8-2 na Bayern Munich kwenye nusu fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Na hapo kocha Setien akatimuliwa na nafasi yake akapewa Ronald Koeman. Lakini wakakumbana na pigo jingine, kwani nyota na nahodha wao, Lionel Messi akawasilisha maombi ya kutaka kuondoka klabuni hapo. Lakini baadaye, raia huyo wa Argentina akaamua kubaki pale Camp Nou, lakini Barcelona walimaliza mwaka bila taji lolote kwa mara ya kwanza kwa kipindi cha miaka 12.

## Extra Time

# WACHEZAJI 10 BORA WA LIGI KUU UFARANSA

**PARIS,** Ufaransa

LIGI Kuu Ufaransa, Ligue 1, ilikuwa ligi ya kwanza kuathirika na mlipuko wa virusi vya corona. Ufaransa ilikuwa moja ya nchi iliyoathirika vibaya na virusi hivyo, hivyo msimu wa Ligi 2019-20 ukalazimika kufutwa na ubingwa wakapewa PSG, ambao walikuwa kileleni mwa msimamo wakati huo.

**Msimu huu mabingwa hao wa Ufaransa, wamejikuta wakiwa kwenye changamoto kubwa ya kuwania taji hilo, kwani Lille na Lyon zimeonyesha zimepania kweli kweli kuwapokonya PSG.**

PSG kwa sasa wapo nafasi ya tatu kwenye msimamo wa Ligi Kuu, Ligue 1, pointi moja nyuma ya Lyon na Lille.

Ligue 1 mara zote imekuwa ikizalisha nyota wakali, kutoka Thierry Henry na Ronaldinho hadi hivi karibuni Eden Hazard. Pia kutumia fedha nyingi kwa klabu kama PSG kumevutia majina ya wachezaji wakubwa duniani kutimkia Ufaransa, na hilo kwa kiasi kikubwa limeongeza ubora wa Ligi ya Ufaransa.

Makala haya yanawaangalia wachezaji 10 bora kwenye Ligi Kuu Ufaransa kwa mwaka 2020, hawa hapa...

### #10. EDUARDO CAMAVINGA (RENNES)

Eduardo Camavinga alijitangaza mwenyewe kwenye soka la dunia msimu uliopita. Kiungo huyo kijana alijipambanua mwenyewe kama mmoja wa nyota wakali wa baadaye duniani kwa kiwango bora alichokionyesha pale Rennes.

Camavinga, ambaye alitimiza umri wa miaka 18, Novemba mwaka jana, alikuwa mmoja wa nguzo kubwa zaidi ya mafanikio ya Rennes waliomaliza katika nafasi ya tatu kwenye msimamo wa Ligue 1 msimu uliopita na kufuzu Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Kiungo huyo alikuwa mchezaji mwenye umri mdogo zaidi kuifungia timu ya Taifa ya Ufaransa bao kwa kipindi cha zaidi ya karne moja mapema mwaka jana.

Camavinga ameonyesha ujuzi na mbinu za kucheza na mpira akilinganishwa na Paul Pogba na Patrick Vieira.

### #9. MOUSSA DEMBELE (LYON)

Moussa Dembele alifurahia zaidi msimu wa 2019-20. Straika huyo wa Ufaransa alikuwa mmoja wa wachezaji muhimu kwa kikosi cha Lyon kilichomaliza nafasi ya saba kwenye msimamo wa Ligue 1.

Dembele alimaliza msimu kama mfungaji bora wa Lyon akitikisa nyavu mara 24 kwenye mashindano yote, akifunga mara 16 kwenye Ligue 1. Pia alifunga mabao mawili kwenye mchezo wa robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya na kuwatoa Manchester City kwenye mashindano hayo.

Dembele ameanza taratibu msimu huu, akiwa anatokea benchi mara kwa mara. Straika huyo hivi karibuni alivunjika mkono kwenye mazoezi na atakuwa nje kwa muda mrefu.

### #8. JONATHAN BAMBA (LILLE)

Jonathan Bamba ameanza msimu huu akiwa na moto balaa. Winga huyo wa Ufaransa amekuwa moja ya nguzo muhimu kwa Lille wakati wakiendelea kuonyesha kiwango cha kuvutia kwenye Ligue 1 msimu huu.

Bamba, alipewa tuzo ya mchezaji bora wa Ligue 1 Oktoba na tayari ameshafunga mabao matano na kutoa pasi za mwisho sita kwa msimu wa 2020-21.

Kama ataendelea kuwa kwenye kiwango hicho, inatarajiwa nyota uyo mwenye umri wa miaka 24 kuzivutia klabu kadhaa za Ulaya kuwania saini yake.

### #7. HOUSSEM AOUAR (LYON)

Ingawa ana umri wa miaka 22, Houssem Aouar amejiimarisha yeye mwenyewe kama mmoja wa viungo bora kwenye Ligue 1. Mfaransa huyo amekuwa kwenye kiwango cha kuvutia zaidi pale Lyon kwa misimu kadhaa iliyopita.

Aouar amekuwa akileta ladha tofauti kwenye nafasi ya kiungo na amekuwa akilinganishwa na gwiji Zinedine Zidane. Aouar pia ameonyesha kwamba ana jicho la goli, mara kwa mara amekuwa na uwezo wa kufunga kila anapopata nafasi ya kufanya hivyo. Tayari ana mabao matatu na pasi za mwisho nne kwenye Ligue 1 msimu huu.

Aouar amekuwa akivumishiwa sana kwenye suala la usajili, huku Arsenal ikiripotiwa kushindwa kumsajili kipindi cha majira ya joto kilichopita. Lakini majaliwa ya Mfaransa huyo yanaonekana dhahiri kwamba yapo mbali na Lyon.

### #6. ANGEL DI MARIA (PSG)

Angel Di Maria alikuwa na mwaka wa kuvutia kwa mabingwa hao wa Ufaransa msimu uliopita. Raia huyo wa Argentina alikuwa mpishi wa kutoa pasi za mwisho kwa PSG msimu uliopita, akiwa na asisti 20 katika mashindano yote.

Di Maria amekuwa mmoja wa wachezaji muhimu sana wa PSG tangu alipohamia hapo akitokea Manchester United. Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 32 pia ni mzuri zaidi kwenye mashambulizi.

Di Maria pia msimu huu ameonekana kuwa na kasi ile ile, kwani tayari ametoa pasi za mwisho tano kwenye Ligue 1 na mbili kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya. Kama PSG watashinda taji msimu huu, tambua kwamba, Di Maria atakuwa amefanya kazi kubwa mno.

### #5. MIKE MAIGNAN (LILLE)

Mike Maignan amekuwa golikipa bora kwenye Ligue 1 mwaka 2020. Mfaransa huyo ndiye moja ya sababu kwa nini Lille wamekuwa wakifanya vizuri zaidi kila wiki katika mechi zake.

Msimu uliopita alishinda tuzo ya Golden Glove baada ya kucheza mechi 12 bila kuruhusu bao katika mechi 28 za Ligue 1. Maignan amekuwa kiongozi mzuri wa kuipanga safu yake ya ulinzi.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 25, tayari amecheza mechi nane kati ya 17 bila kuruhusu bao msimu huu, wakati Lille wakiwa nafasi ya pili kwenye msimamo wa Ligue 1.

### #4. MEMPHIS DEPAY (LYON)

Memphis Depay amekuwa mmoja wa wachezaji hatari zaidi duniani tangu alipojiunga na Lyon. Raia huyo wa Uholanzi ameng'ara kwenye Ligue 1 tangu alipotua hapo akitokea Manchester United.

Nyota huyo alikosa kipindi kikubwa cha msimu uliopita kutokana na majeruhi, lakini alifunga mabao tisa kwenye mechi 11 za Ligue 1. Depay bado yupo kwenye kiwango bora msimu huu, akiwa amefunga mabao nane na kutoka pasi za mwisho nne kwenye mechi 13 alizoanza kwa Lyon kwenye Ligue 1.

Kiwango cha Mholanzi huyo kimemfanya kuhusishwa na mpango wa kutakiwa kule Barcelona, huku kocha wa sasa wa klabu hiyo ya Catalunya, Ronald Koeman ni mmoja wa shabiki mkubwa wa Depay.

### #3. WISSAM BEN-YEDDER (MONACO)

Wissam Ben-Yedder amekuwa straika bora wa Ligue 1 kwa mwaka 2020. Mfaransa huyo kiwango chake kwa Monaco kimekuwa kisichoshuka na ndio maana kikosi hicho cha kocha, Nico Kovac kimekuwa kikifanya vizuri.

Ben-Yedder alikuwa mmoja wa wafungaji bora wa Ligue 1 msimu uliopita akitikisa nyavu mara 18, na uwezo wake wa kufunga umeonyesha ishara ya kutokushuka. Mshambuliaji huyo Mfaransa tayari ana mabao saba na pasi za mwisho nne msimu huu, na amekuwa na upatina mzuri na Kevin Volland kwenye safu ya ushambuliaji ya Monaco.

### #2. NEYMAR (PSG)

Si mengi ya kuzungumzwa hapa, kwani Neymar ni mchezaji wa daraja la juu kabisa duniani. Mshambuliaji huyo wa PSG ameifanya Ligue 1 kuonekana bora tangu alipojiunga na mabingwa hao wa Ufaransa akitokea Barcelona.

Kitu pekee kinachomfanya Neymar kutokuwa kwenye orodha ya wafungaji bora ni rekodi yake ya kuwa majeruhi mara kwa mara. Neymar kamwe hajawahi kucheza zaidi ya mechi 20 mfululizo za Ligue 1 kwa msimu mmoja pale PSG tangu alipojiunga na klabu hiyo mwaka 2017.

Raia huyo wa Brazil alimaliza msimu uliopita akiwa na mabao 13 na pasi za mwisho sita kwenye ligi na tayari ana mabao matatu na pasi za mwisho nne katika mechi saba msimu huu.

### #1. KYLIAN MBAPPE (PSG)

Kylian Mbappe amekuwa mmoja wa nyota wakubwa zaidi wa Ligue 1 tangu alipochomoza mwaka 2015 akiwa pale Monaco. Mshambuliaji huyo wa Ufaransa anaonekana kuimarika na kuwa bora kila msimu na tayari anatajwa kama mmoja wa wachezaji bora kabisa katika sayari hii.

Nyota huyo mwenye umri wa miaka 22, msimu uliopita alitwaa Kiatu cha Dhahabu kwa kuwa mfungaji bora msimu uliopita akitikisa nyavu mara 18 katika mechi 17 wakati PSG walipobeba taji la Ligue 1. Mfaransa huyo ameendelea kuwa kwenye kiwango cha kuvutia msimu huu, akifunga mara 12 katika mechi 13 za Ligue 1.

Mbappe amekuwa mchezaji bora wa Ligue 1 mwaka huu na straika huyo kijana anaonekana bado ana moto sana. Ikichukuliwa kwamba bado ni kijana, Mbappe ana na nafasi ya kufika mbali zaidi.


NEYMAR
MBAPPE

## Nukuu

"MESSI anafunga goli na kushangilia. Cristiano anafunga goli na kupozi kama vile yupo kwenye tangazo la biashara la shampoo," **Diego Maradona enzi za uhai wake akichambua ushangiliaji wa Cristiano Ronaldo na ule wa Lionel Messi.**



"Kwa miaka yote nilikuwa na vita kubwa na Ashley Cole, hakupi sekunde ya kupumua. Alikuwa mchezaji hodari sana wakati akiwa kwenye ubora wake, haraka, mgumu katika kukabiliana naye. Ulijua kamwe usingekuwa mchezo rahisi," **Straika wa Juventus, Cristiano Ronaldo, akieleza beki aliyempa tabu sana uwanjani.**



"Kuweka alama kwa mchezaji kuwa kufuatilia hakunisumbui- unajua kwamba kutakuwa na mechi ngumu na inaweza kuwa ya kushangaza kuwa na mtu karibu yako kila wakati. Kwa kweli, haikunitokea mara nyingi. Hainisumbui, lakini ni ya ajabu. Pablo Maffeo wa Girona [alikuwa mtu mwenye alama kali zaidi]. Hiyo ilikuwa kali! "**Nyota wa Barcelona, Lionel Messi, akieleza beki hatari zaidi kwake.**



# NYOTA 7 WALIOREJEA TENA LIGI KUU BARA



DEOGRATIUS MUNISHI (DIDA)

**Na Adam Fungamwango**

WAKATI dirisha dogo la usajili likiwa limefunguliwa, tumeanza kuona baadhi ya wachezaji ambao waliwahi kucheza Ligi Kuu Tanzania Bara, wamerejea.

**Wachezaji hao ni wale ambao baada ya kucheza walipumzika nyumbani, walikuwa hawapati nafasi ya kucheza kwenye timu walizokuwa wakizitumikia na wametolewa kwa mkopo, au walikuwa wakicheza Ligi Daraja la Kwanza Tanzania Bara.**

Tayari baadhi ya wachezaji hao wameshaanza kusajiliwa na timu mbalimbali za Ligi Kuu wakikumbuka mchango wao walioutoa huko nyuma, lakini uzoefu wao ukionekana kuhitajika zaidi kwa ajili ya kuimarisha vikosi. Je, unawajua?...

### #1. DEOGRATIUS MUNISHI 'DIDA'- IHEFU

Ni golikipa mkongwe Tanzania, akiwahi kuzichezea klabu zote kubwa nchini, Simba, Yanga, Mtibwa Sugar na Azam FC. Amesajiliwa na Ihefu kwa mkataba wa mwaka mmoja kwenda kulinda lango la timu hiyo ambalo linaonekana bado halijapata kipa imara.

Makosa ya mara kwa mara ya kipa, Andrew Kayuni, yamewafanya viongozi wa klabu hiyo kumsaka kipa huyo ambaye alikuwa amejikalia zake nyumbani, na kumsimamisha langoni. Alianza kuonekana kwenye mechi dhidi ya Yanga na pamoja ya kufungwa mabao 3-0, lakini aliokoa mabao mengi mno. Anaonekana bado ana uwezo mkubwa na ataisaidia timu hiyo. Kabla ya hapo, Dida alikuwa Lipuli ambayo ilishuka daraja, msimu wa 2019/20 aliidakia Simba.

### #2. YUSUPH MLIPILI- KAGERA SUGAR

Kagera Sugar imetangaza kumsajili beki kisiki wa zamani wa Simba, Yusuph Mlipili kwa mkataba wa mwaka mmoja. Kwa kipindi cha nusu msimu alikuwa huru, akiwa ameachwa na klabu ya Simba.

Klabu hiyo imetangaza kumsajili mchezaji mmoja tu kwenye kipindi hiki cha dirisha dogo, Mlipili ambaye aliyekuwa hana timu kwa sasa. Mchezaji huyo alijiunga na Toto African mwaka 2015, hadi mwaka 2017 alipojiunga na Simba, akiwa beki tegemeo kwenye kikosi hicho wakati huo.

Mlipili aliachwa na Simba baada ya msimu uliopita kumalizika, kutokana na kukosa namba kwenye kikosi hicho. Mara ya mwisho kwa mchezaji huyo kucheza kwa kiwango cha juu ni mechi ya Kombe la Shirikisho Afrika (CAF, kati ya Simba na Al Masry ya Misri kwenye mechi zote mbili za nyumbani na ugenini zilizochezwa Machi 2018.

### #3. JUMA MAHADHI-IHEFU

Anakumbukwa sana mwaka 2016, alipoisumbua ngome ya TP Mazembe kwenye mechi ya Ligi ya Mabingwa Afrika Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam, timu yake ya Yanga ikilala kwa bao 1-0. Ndiyo kwanza ilikuwa imemsajili kutoka Coastal Union. Baada ya hapo uwezo wake ulionekana kupungua, lakini pia majeraha yanaanza kumuandama na kukaa nje kwa muda mrefu.

Hata aliporejea hakupata namba kwenye kikosi. Amejiunga na Ihefu kwa mkopo na mechi yake ya kwanza kucheza ilikuwa ni dhidi ya waajiri wake Yanga na kwa mara ya kwanza akaonekana uwanjani baada ya muda mrefu.

### #4. KELVIN YONDANI- POLISI TANZANIA

Beki huyu mkongwe amesajiliwa na Polisi Tanzania kipindi hiki cha dirisha dogo, akiwa kama mchezaji huru. Kelvin Yondani, aliachwa na Yanga msimu uliopita na msimu huu ilikuwa nusura ajiunge na Ndanda FC, lakini ilishindikana.

Kukaa kwake nusu msimu bila kucheza soka kulikuwa kunawaumiza baadhi ya mashabiki wa soka nchini, hasa wakiangalia aina ya baadhi ya mabeki wa Ligi Kuu nchini walivyokuwa na makosa mengi. Awali, timu ya JKT Tanzania ndiyo ilioonyesha nia ya kutaka kumchukua, lakini sasa ameibukia Polisi Tanzania.

### #5. JOSEPH MAHUNDI- IHEFU

Ni mchezaji wa zamani wa klabu za Coastal Union na Azam FC. Naye alikuwa kimya tangu kuanza kwa msimu huu. Hata hivyo, ameibukia Ihefu FC na alianza kuonekana kwenye mechi ambayo timu yake ilicheza dhidi ya Yanga. Ni mmoja kati ya wachezaji waliorejea kwenye Ligi Kuu kipindi hiki cha dirisha dogo.

### #6. MRISHO NGASSA- GWAMBINA FC

Winga machachari wa zamani wa klabu za Simba, Yanga, Azam, Mbeya City na klabu mbalimbali za nje ya nchi, Mrisho Ngassa, amejiunga na Gwambina kipindi hiki cha dirisha dogo.

Ngassa, anajiunga na timu hiyo akitokea Ndanda inayoshiriki Ligi Daraja la Kwanza Tanzania Bara. Mara ya mwisho aliichezea Yanga, hivyo sasa anaingia kwenye orodha ya wachezaji wanaorejea tena kwenye Ligi Kuu.

### #7. EDWARD CHRISTOPHA- COASTAL UNION

Juzi Coastal Union ilimtangaza mchezaji wa zamani wa Simba na Kagera Sugar, Edward Christopha kuwa imemsajili kwa mkataba wa miezi sita. Winga huyo ambaye ni zao la kikosi cha pili cha Simba, mara ya mwisho alisikika akiwa Kagera Sugar msimu mmoja uliopita.

Naye ni mmoja wa wachezaji ambao wamerejea tena kwenye Ligi Kuu, kuongeza nguvu kwenye timu inayohitaji huduma za wachezaji wenye uzoefu.

**JE, WAJUA?**



HARRY Kane ni mchezaji aliyetoa pasi za mwisho nyingi (pasi za mwisho 10) kwenye Ligi Kuu England msimu huu kuliko Jack Grealish (pasi za mwisho saba), wakati pia mchezaji wa mwisho wa Aston Villa kutoa zaidi ya pasi saba za mwisho kwenye Ligi Kuu England kwa msimu, alikuwa Ashley Young msimu wa 2010-11 (10).



# Askofu Chande akemea biashara kusafirisha binadamu

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

ASKOFU mstaafu wa Kanisa la EAGT, Ipagala mkoani Dodoma, Mchungaji Dk. Evance Chande, ameiomba serikali kuchukua hatua kali za kisheria zitakazokomesha biashara ya kusafirisha binadamu na kuwaficha wahamiaji wanaoingia nchini kinyume cha sheria.

Dk. Chande aliyasema hayo alipokuwa akihubiri kwenye ibada ya mwaka mpya ambayo ilikuwa maalumu kwa ajili ya kumshukuru Mungu kwa kuwavusha waumini mwaka 2020 na kuingia mwaka mpya wa 2021.

Alisema, kitendo cha kuwasafirisha na kuwaficha majumbani wahamiaji haramu ambao wanaoingia kinyume na sheria za nchi kinachofanywa na baadhi ya Watanzania ni usaliti kwa taifa na kutaka wanaobainika ni serikali iwachukulie hatua kali za kisheria.

Pia, alisema kuwa Tanzania siyo nchi ya kupitisha na kuwaficha wahamiaji na kwamba wanaofanya biashara hiyo haramu ni sawa na wahujumu uchumi na wanasaliti wa taifa ambao wanaweza kusababisha kutoweka kwa amani.

Alisema kutokana na hali hiyo, watu hao wanastahili kupewa adhabu kali ambayo itakuwa fundisho kwa wengine.

Dk. Chande katika mahubiri yake pia aliwaomba Watanzania kuendelea kumwombea Rais John Magufuli pamoja na timu yake ili Mungu awafanikishe kwenye utendaji wao wa kazi ya kuwatumikia kwa ajili ya maendeleo ya nchi.

Katika mahubiri yake ambayo yalibeba ujumbe maalumu wa kaulimbiu "Mwaka 2021 ni wa Ushindi" aliwaomba Watanzania kuendelea kulinda rasilimali zilizopo nchini, ili zikafaidishe kwa watu wote.

Alikemea baadhi ya Watanzania wenye tabia ya kuwanyoshea vidole viongozi wa serikali na kuwataka kuwa mabalozi wa kuwatetea na kuwaombea ili waweze kufanya kazi zao kwa amani na utulivu.

Aliwaomba Watanzania kufanya kazi za uzalishaji kwa bidii ili uchumi ukue na viwanda viongezeke pamoja na ajira.

Katika ibada hiyo ya shukrani aliwaombea mahitaji mbalimbali yakiwamo kuombea serikali, watumishi wake, wakulima, wafugaji, wanafunzi wa kada mbalimbali, wanahabari, wajane na yatima, wageni wa kutoka nje ya Tanzania pamoja na kazi ya kanisa.



Gari aina ya Scania T.994 DCV na tela namba T.861 BXS jana likiwa limeanguka katikati ya barabara kuu ya kuelekea mpakani Kabanga Ngara nchini Burundi na kusababisha baadhi ya magari kushindwa kwenda nchini humo kwa muda. **PICHA: SHABAN NJIA**

# TARILI yashauri wafugaji kutumia ng'ombe chotara

**Na Renataha Msungu,** MPWAPWA

TAASISI ya Utafiti wa Mifugo nchini (TARILI), Kituo cha Mpwapwa imewashauri wafugaji kutumia ng'ombe dume aina ya chotara Mpwapwa, ili ufugaji uwe wa tija.

Kaimu Mkurugenzi wa kituo hicho, Aluna Chawala, alisema hayo wakati akielezea faida za ng'ombe chotara Mpwapwa, anazoweza kupata mfugaji anayefuga kiasili akitumia madume hayo.

Dk. Chawala alisema kituo hicho kinafanya jitihada za kuhimiza wafugaji kutumia teknolojia ya kuchanganya dume la chotara Mpwapwa na ng'ombe jike wa asili ili kubadilisha aina ya mifugo waliokuwa nayo na kupata mbegu za chotara Mpwapwa.

Alisema, sifa kubwa za ng'ombe chotara Mpwapwa kwa mfugaji hutoa maziwa mengi kwa siku, kuanzia lita 10 hadi 16 kulingana na mazingira anayotunzwa.

"Kituo kinajitahidi kusambaza teknolojia hiyo ya kuchanganya madume ya chotara Mpwapwa kwa wafugaji, kwa sababu wamejiridhisha aina hiyo ya ng'ombe wanaweza kuvumilia mazingira ya ukame kama walivyo wengine wa asili," alisema Dk. Chawala.

Kadhalika, alielezea faida nyingine ya chotara Mpwapwa kuwa ni uwezo wa kutoa nyama nyingi pia anavumilia mazingira ya ukame kama walivyo ng'ombe wa asili. "Chotara Mpwapwa ana faida kubwa sana kwa mfugaji, wakitumia teknolojia ya kuchanganya mifugo yao ya asili na chotara Mpwapwa itawasaidia kubadilisha ufugaji wanaofanya," alisema Dk. Chawala. Naye, mtafiti kutoka idara ya utafiti wa ng'ombe, Deogratius Masao, alisema teknolojia ya kuzalisha ng'ombe chotara Mpwapwa ni kuwajengea uwezo wafugaji waweze kufanya ufugaji wenye tija ambao utawainua kiuchumi.

Masao, alisema kituo hicho kimejitahidi kuzishawishi halmashauri kutoka sehemu mbalimbali kununua ng'ombe hao kwa ajili ya kupeleka kuwasambazia wafugaji ili nao waanze kutumia teknolojia hiyo ambayo inafaida kubwa kwa wafugaji.

Alisema wamekuwa wakipeleka teknolojia hiyo katika vijiji mbalimbali ikiwamo kuwapa elimu ya namna ya ufugaji wenye tija unavyomuinua mfugaji kutoka hatua moja kwenda nyingine.

Kituo hicho kimeishukuru serikali kupitia Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia kufadhili miradi mbalimbali ya utafiti ambao umesaidia kubaini ng'ombe aina ya chotara Mpwapwa.

# Wakumbushwa umuhimu wa kupanda miti

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

ASKOFU mstaafu wa Kanisa la EAGT New Jerusalem Ihumwa Dodoma, Robert Mangwela, amewaomba wakazi wa mikoa ya Kanda ya Kati kuzitumia mvua zinazoendelea kunyesha kupanda miti kwa wingi ili kutunza mazingira.

Alitoa ushauri huo jana wakati alipokuwa akizungumza na waumini wa kanisa hilo kwenye upandaji miti kanisani hapo.

Akizungumza kwenye upandaji miti huo ulioambatana na ibada ya maalumu ya kuwaombea watoto iliyofanyika kanisani hapo, alisema pamoja na ulimaji wa mashamba pia mvua hizo zitumike kwa upandaji wa miti kwenye maeneo mbalimbali na yale ambayo yametengwa kwa ajili ya uhifadhi na kwenye uoto wa asili.

"Ninawaomba Watanzania wezangu kwenye mikoa ambayo mvua zinaendelea kunyesha tutumie fursa hii pia kwa kupanda miti kwenye maeneo mbalimbali ikiwamo milimani, kwenye vyanzo vya maji na uoto wa asili ili tuweze kutunza mazingira yetu," alisema.

Alisema utunzaji wa mazingira ni maelekezo kutoka kwa Mungu kwa maana imeandikwa kuwa baada ya kuumba kwa kila kitu anatengeneza bustani na kuweka kila kitu na kumwambia Adamu aitunze," alifafanua.

Aliwashauri wakulima kutumia mvua inayoendelea kunyesha kwenye mikoa mbalimbali, kupanda mazao ambayo yanaendana na sehemu husika.

Awali, akihubiri kwenye ibada hiyo pia aliwataka wazazi na walezi kuwajibika kuwalea watoto wao, katika misingi ya maisha ya kiuadilifu ili kupata taifa lenye viongozi waaminifu kwa ajili ya nchi yao.

Alisema ili nchi iweze kuwa na viongozi waadilifu na wacha Mungu ambao wanachukia wizi, dhuluma, uonenu, wala rushwa na mafisadi ni muhimu wazazi na walezi wakawajibika kuwawekea misingi mizuri ya uadilifu.

Mangwela, alisema wazazi na walezi wengi wao wamekuwa mbali na watoto wao kimalezi, jambo ambalo limesababisha kuwapo kwa mmonyoko wa uadilifu na maadili.

"Kanisa hili tunafanya ibada hii maalumu ya kuwaweka watoto wetu wakfu ikiwa kwa mwaka 2021 kama ishara ya kuwakabidhi watoto hawa mikononi mwa Mungu, lakini pamoja na ibada hii nawasihii wazazi na walezi wezangu isiwe sababu ya kuwaacha watoto hawa bila kuwajengea miongozo na misingi sahihi ya hofu ya Mungu.

"Wapo wazazi ambao wamekuwa mbali sana na watoto wao jambo ambalo linasababisha familia nyingi kutopenda tamaduni za kitanzania kuwa na tabia ambayo haina utukufu mbele za wanadamu wala Mungu," alisema.







Naibu Waziri wa Maji, Mhandisi Maryprisca Mahundi (kulia), akitoa maelekezo kwa watendaji wa Wakala wa Usambazaji Maji Vijijini (RUWASA), Wilaya ya Mbarali, mkoani Mbeya, kuhusu mradi wa maji ya kisima wa Ilongo Group ambao umetelekezwa kwa muda mrefu. **PICHA: NEBART MSOKWA.**

# Avunja bodi tuhuma kushindwa kufikishia wananchi huduma maji

**Na Nebart Msokwa,** MBARALI

NAIBU Waziri wa Maji, Mhandisi Maryprisca Mahundi, ameivunja Bodi ya Mamlaka ya Maji ya Mji Mdogo wa Rujewa, wilayani Mbarali katika Mkoa wa Mbeya kwa tuhuma za kushindwa kuisimamia mamlaka hiyo kufikisha huduma ya maji kwa wananchi.

Aidha, amemwagiza Mkurugenzi Mkuu wa Wakala wa Usambazaji Maji vijijini (RUWASA), Clement Kivegalo, kumwondoa Meneja wa Wakala huo, Wilaya ya Mbarali, Job Mwakasala, kwenye nafasi hiyo kwa tuhuma za kushindwa kusimamia miradi ya maji na kutoa taarifa za uongo kuhusu miradi hiyo.

Alifanya uamuzi huo juzi alipofanya ziara ya kukagua utekelezaji wa miradi ya maji wilayani humo na kushuhudia wananchi wakipata shida ya kupata maji ya bomba huku miradi mingi ikiwa imetelekezwa na hata iliyokamilika ikiwa haitowi maji.

Akizungumza baada ya kukagua miradi hiyo, alisema Bodi ya Maji ya Rujewa haijatekeleza majukumu yake ipasavyo na hivyo kusababisha miradi yote inayohudumia mji huo ikiwa haitowi maji, huku wananchi wakinywa maji ya kwenye mifereji ya skimu za umwagiliaji.

Mahundi alisema alibaini kuwa Meneja wa RUWASA Wilaya hiyo alitoa taarifa za uongo kuhusu hali ya upatikanaji wa maji wilayani humo kwa kusema kuwa ni asilimia 69.9 wakati uhalisia unaonyesha ni chini ya asilimia 30.

Vilevile alisema Meneja wa RUWASA wa wilaya hiyo, alikabidhiwa fedha kwa ajili ya utekelezaji wa miradi mbalimbali ukiwamo wa Ruduga-Mawindi unaotarajiwa kugharimu zaidi ya Sh. bilioni 12 tangu mwezi Agosti mwaka jana, lakini hakuna utekelezaji uliofanywa huku wakiwa wametelekeza vifaa yakiwamo mabomba kwa zaidi ya miezi minne.

"Miradi mingi ya maji hapa Mbarali ni 'kichefuchefu' na ni ya ovyo kupita kiasi, hii ni kutokana na uzembe wa watendaji wa RUWASA wilayani hapa, sasa nakuagiza DG (Mkurugenzi Mkuu), umwondoe meneja wa hapa na ikiwezekana hata watendaji wengine waondolewe ili tuanze na timu mpya," alisema Mahundi na kuongeza:

"Nimeivunja Bodi ya Maji ya Mji wa Rujewa kuanzia leo (juzi) na nataka iundwe nyingine, isije ikatokea wakati wa kuundwa bodi mpya akaingizwa mjumbe maana hana kitu kipya cha kutuletea."

Mkuu wa Wilaya ya Mbarali, Reuben Mfune, alisema wilaya hiyo inakabiliwa na tatizo kubwa la upatikanaji wa maji ya bomba tofauti na taarifa zinazotolewa na watendaji wa RUWASA kwa viongozi wanaotembelea wilaya hiyo.

Alisema hata yeye alikuwa anaamini kuwa hali ya upatikanaji wa huduma hiyo ni nzuri, lakini alibaini kuwa ni mbaya baada ya kufanya ziara kwenye maeneo mbalimbali na kukuta wananchi wanalalamika mabomba hayatoi maji.

"RUWASA wanasema hali ya upatikanaji wa maji kwenye wilaya hii ni asilimia 69.9, lakini uhalisia wake ni chini ya asilimia 30 japo miradi ipo na mabomba yapo, mengi ya mabomba hayatoi maji," alisema Mfune.

Kwa upande wake Mkurugenzi Mkuu wa RUWASA, Mhandisi Kivigelo, aliahidi kupeleka timu ya wahandisi kutoka katika mikoa mingine kwenda kutekeleza miradi iliyokwama wilayani humo kwa maelezo kuwa hali ni mbaya.

Alisema watendaji wake walikuwa wanamdanganya na hivyo akasisitiza kuwa atahakikisha miradi hiyo inakamilika na wananchi wanapata huduma huku akiahidi kutekeleza agizo la Naibu Waziri.

# Wazee waomba jiji kuboresha mazingira uwekezaji

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

UMOJA wa wazee ambao ni wadau wa maendeleo mkoani Mbeya, umeuomba uongozi wa Jiji la Mbeya, kuboresha mazingira ya uwekezaji kwenye sekta mbalimbali hasa majengo, ili kuondoa sura ya jiji hilo ambayo imejaa majengo yaliyochakaa na vichaka maeneo ya mjini.

Wazee hao zaidi ya 20, walifika katika Ofisi ya Mkurugenzi wa Jiji la Mbeya, Amede Ng'wanidako, juzi, kuwasilisha maoni yao kuhusu uwekezaji na kusema ni vyema majengo ya zamani yaliyochakaa yakavunjwa na kujengwa mapya.

Akizungumza kwenye kikao hicho, Diwani mstaafu wa Kata ya Nzovwe, Gerson Mwandete, ambaye aliongoza kata hiyo kuanzia mwaka 1994 mpaka 2004 aliomba eneo lililokuwa Soko Kuu la Uhindini ambalo liliungua mwaka 2010 pajengwe jengo refu na la kisasa ili kupendezesha mji.

Alisema serikali inatakiwa kuwanyang'anya wamiliki wa viwanja ambao hawajaviendeleza tangu serikali ya awamu ya kwanza na wapewe wawekezaji wengine watakaoviendeleza ili kuondoa vichaka mjini.

Alivitaja baadhi ya viwanja hivyo kuwa ni pamoja na kile kinachomilikiwa na Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa watumishi wa Umma (PSSSF), kilichopo katika Kata ya Sisimba, katikati ya jiji hilo ambacho kimegeuka kichaka.

Vilevile, alisema katika eneo la RRM lililopo karibu na stendi ya mabasi ya Nanenane ambalo lina ukubwa wa zaidi ya ekari 10 ambalo halijaendelezwa kwa muda mrefu limegeuka kuwa maficho ya vibaka.

"Haya maeneo yanatakiwa wapewe wawekezaji wengine ambao wanaweza wakajenga shule za kisasa, vyuo vikuu, hospitali na hoteli za kisasa, lakini sasa hivi haya maeneo yanakuwa kama yametelekezwa," alisema Mwandete.

Naye Mbunge mstaafu wa Jimbo la Mbeya, Mwaiseje Polisya, aliomba shule za kidato cha tano na sita katika jiji ziongezeke zifikie 20 ili kuongeza idadi ya vijana wanaofikia ngazi hiyo.

Alisema katika kipindi hiki ambacho serikali inahimiza uchumi wa viwanda, idadi ya wasomi inatakiwa kuongezeka ili kuwa na wataalamu wengi wa kuendesha viwanda hivyo.

Naye Mkuu wa Shule ya Sekondari ya Mwakaleli, wilayani Rungwe, mstaafu Andalalisye Mwaihabi ambaye aliiongoza shule hiyo kati ya 1982 na 1994, alisema wazee wanaunga mkono juhudi za serikali kuibadili Tanzania hasa katika mfumo wa uchumi.

# Waomba kuboreshewa barabara kupata huduma

**Na Nebart Msokwa,** BUSOKELO

WANANCHI wa Kijiji cha Bujingijila katika Halmashauri ya Busokelo mkoani Mbeya, wameiomba serikali kuwasaidia kuboresha barabara inayounganisha kijiji hicho na Makao Makuu ya Kata ya Kandete ili kuwarahisisha upatikanaji wa huduma.

Wakizungumza na Nipashe, wananchi hao walisema barabara hiyo imeharibika na kutopitika hali inayowasababishia kukosa huduma muhimu zinazopatikana kwenye kata.

Mmoja wa wananchi hao, Ambindwile Malundi, alisema barabara hiyo ni mbovu hasa kipindi cha mvua kwa kujaa makorongo na baadhi ya sehemu kuwa na madimbwi ambayo yanasababisha wenye vyombo vya usafiri kushindwa kupitisha vyombo vyao.

Alisema katika eneo hilo wananchi wanalima mazao mbalimbali, lakini wanashindwa kusafirisha kutokana na ubovu wa barabara hiyo na kuomba wasaidiwe kuboresha angalau ijengwe kwa kiwango cha changarawe.

"Sisi huku tunalima maparachichi, miti na viazi, sasa kutokana na ubovu wa barabara hii, tunaiomba serikali itukumbuke, hii barabara pia inaenda kwenye mradi mkubwa wa maji wa Kandete ambao ni muhimu, lakini haufikiki kirahisi kwa sasa kutokana na barabara hii," alisema Malundi.

Naye Geoge Saimon, alisema wanalazimika kuwabeba wagonjwa kwenye machela kuwapeleka hospitalini ama kuwasafirisha kwa kutumia pikipiki na baiskeli kwa sababu magari hayafiki kipindi cha mvua.

Alisema kitendo hicho kinawafanya wajione wamesahaulika na kudai kuwa barabara hiyo inakwamisha shughuli zao za maendeleo ikiwamo kilimo na afya.

Kwa upande wake Mwenyekiti wa Halmashauri ya Busokelo, Anyosisye Njobelo, alisema wanatarajia barabara hiyo ijengwe kupitia Wakala wa Barabara za Mijini na Vijijini (TARURA) baada ya mvua kupungua.

Alisema serikali kwa sasa imekuwa ikijaribu kuhakikisha miradi mbalimbali inayowahusu wananchi inatekelezwa ili wananchi wapate huduma kwa urahisi.



HABARI ZANZIBAR

# Maalim Seif ataja siri umoja, mshikamano

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MAKAMU wa kwanza wa Rais wa Zanzibar, Maalim Seif Sharif Hamad, amesema uadilifu katika kuwahudumia wananchi umesababisha kujenga umoja na mshikamano nchini.

Alisema wenye mamlaka ya kuwahudumia wananchi kuanzia masheha hadi viongozi wakuu wa serikali wakiwa waadilifu amani itaendelea kudumu.

Alitoa kauli hiyo akiwa katika Shule ya Sekondari Uweleni, kiswani Pemba, alipokuwa akizungumza na makundi maalum ya wananchi hao.

"Tunataka tuhakikishe katika serikali yetu kusiwapo na ubaguzi, kila mwenye haki apate bila ya ubaguzi," alisema Maalim Seif.

Aidha, aliwataka viongozi wa mikoa, wilaya hadi shehia kufanyakazi kwa kuifuata Katiba ambayo wameapa kuilinda na kuitetea.

"Kama mkiifuata Katiba mtakuwa waadilifu na hakutakuwa na ubaguzi katika kutekeleza majukumu yenu," alisema Maalim Seif.

Alisema wakati umefika kwa Wazanzibari wote kuwa wamoja wenye kufanya kazi kwa ushirikiano ili kuiweka nchi vizuri kwa kipindi kifupi tokea serikali ya awamu ya nane kukaa madarakani.

Alisema Zanzibar bila ya maridhiano ya pamoja maendeleo hayawezi kupatikana, hivyo ni vyema kila mmoja kuthamini maridhiano yaliyopo.

"Nampongeza Dk. Mwinyi, kwa uamuzi wake, haikuwa rahisi kuungana kwetu bali tumeongozwa na maslahi ya Zanzibar na matakwa ya katiba yetu," alisema Maalim Seif.

Vilevile, aliwataka wananchi hao kuacha tofauti zao za kisiasa na kueleza kuwa ndizo zinazoleta mifarakano na badala yake waungane kwa kuleta maendeleo.

Naye Mkuu wa Mkoa wa Kusini Pemba, Mattar Zahor Masoud, aliwataka wananchi hao kuunga mkono maridhiano waliyopitishwa na viongozi ili kufikia mustakabali uliokusudiwa.

Alisema umoja ndiyo silaha ya mafanikio kwa wananchi na taifa lolote, hivyo kila mmoja ana haki na wajibu wakuona Taifa linapiga hatua za haraka kimaendeleo.

Kwa upande wao wananchi waliipongeza serikali kwa kuondoa chuki, visasi na mifarakano miongoni mwa Wazanzibari.

Wananchi hao waliahidi kushirikiana na serikali kwa maslahi ya Zanzibar na watu wake na kuweka mbali itikadi zao za kisiasa.



Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleiman, akimfariji mmoja wa wanamichezo waliopata ajali ya kugongwa na gari, Migombani wakiwa mazoezini. **PICHA: OMPR**

# Hemed ataka uchunguzi ajali wanamichezo 14

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MAKAMU wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleiman Abdulla, amemwagiza Kamishna wa Polisi Zanzibar kufanya uchunguzi wa kina na wa haraka utakaobainisha chanzo cha ajali iliyosababisha wanamichezo waliokuwa mazoezini katika eneo la Migombani kugongwa na gari.

Ajali hiyo iliyotokea juzi asubuhi eneo la Migombani Mjini Unguja wakati wanamichezo hao 14 wakiwa kwenye mazoezi.

Abdulla alitoa agizo hilo wakati alipowatembelea majeruhi hao katika Hospitali ya Mnazi Mmoja, Mjini Unguja.

Aliwataka madereva wanapoendesha vyombo vya moto lazima waelewe na kuzingatia kwamba barabara zinatumiwa na watu wote hata wale wanaotembea kwa miguu, kuzingatia sheria za barabarani.

Alisema serikali isingependa kuona kunakuwapo na matukio ya ajabu yanayotishia uhai na maisha ya wananchi yakihusishwa na uzembe unaofanywa na baadhi ya madereva kwa kutokuzingatia sheria, miongozo na kanuni zilizowekwa za matumizi sahihi ya barabara.

Aidha, aliwapongeza madaktari na watendaji wa Hospitali Kuu ya Mnazi Mmoja kwa jitihada walizochukuwa za kuwahudumia wanamichezo hao na kuridhika na hatua hiyo iliyompa faraja kubwa.

Naye Kaimu Mkurugenzi wa Hospitali ya Mnazi Mmoja, Dk. Marijani Msafiri, alisema wanamichezo 14 wamepokelewa hospitalini hapo mapema asubuhi juzi na kuanza kupata huduma za matibabu.

Alisema kati ya wagonjwa hao 14, watano wamelazwa kwa uchunguzi zaidi ya hali zao, wawili wamefanyia vipimo zaidi, wawili wamepelekwa chumba cha upasuaji na watano wamepatiwa huduma na kuruhusiwa kurejea nyumbani.

Mmoja kati yamajeruhi hao akizungumza na Nipashe alisema gari hiyo iliyokuwa ikiendeshwa kwa mwendo wa kasi iliivamia gari iliyokuwa pembezoni mwa barabara katika eneo la Migombani Jeshini na kusereka na kuwavamia wakiwa wanatembea kwenye mazoezi yao ya kawaida.

# Wanne mbaroni kusafirisha magendo

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WATU wanne wanashikiliwa na Jeshi la Polisi Mkoa wa Mjini Magharibi Unguja kwa tuhuma za kusafirisha mizigo kwa njia ya magendo, ikiwamo sukari viroba 12.

Akizungumza na waandishi wa habari, Kamanda wa Polisi wa mkoa huo, Kamishna Msaidizi wa Polisi, Awadh Juma Haji, alithibitisha kukamatwa kwa watu hao katika ufukwe wa Funguni na bandari bubu ya Dimani.

Aliwataja waliokamatwa katika Bandari ya Bweleo Desemba 27 majira ya saa 12:45 jioni ni Fahmi Ali Khamis (27), mkazi wa Miembeni na Ali Hamza Mwinyi (50), mkazi wa Bweleo ambaye ni mfanyabiashara.

Alisema watuhumiwa hao walikamatwa wakiwa na runinga 14 pamoja na redio nne kubwa wakisafirisha kwa njia ya magendo kwa kutumia bandari bubu, kinyume na sheria na taratibu za serikali.

Kamanda Awadh alibainisha kuwa katika tukio hilo pia walikamata gari mbili zenye namba za usajili Z. 276 JW P/V aina ya Alfard rangi ya silva na gari yenye namba za usajili Z 993 KU aina ya Noah rangi nyeupe, zote zikiwa zinahusika katika kusafirisha mzigo huo.

Aidha, alisema tukio lingine liliwahusisha Shaibu Yussuf Mmanga (30) na Khatib Hamdu Masiku (35), ambao ni wafanyabiashara wakazi wa Mafia Mkoa wa Pwani, ambao walikamatwa Desemba 28, mwaka jana, majira ya saa 5:00 usiku maeneo ya Malindi Mkoa wa Mjini Magharibi Unguja.

Alisema watuhumiwa hao walikamatwa wakiwa wanasafirisha sukari viroba 12 zenye ujazo wa kilogramu 50 kila moja wakiwa na lengo la kuisafirisha nje ya nchi kwa kutumia njia ya magendo, ili kukwepa kulipa kodi ya serikali jambo ambalo ni kosa kisheria.

Mbali na matukio hayo, Kamanda Juma Haji alisema mengine yaliwahusisha watuhumiwa wengine watatu kwa tuhuma za kuwanyang'anya watalii mali zao.

# BAVICHA yaja mkakati mpya 2021

**Na Elizabeth Zaya**

BARAZA la Vijana la CHADEMA (BAVICHA), limetangaza kuwa linajipanga mwaka huu, kuanzisha vuguvugu la kudai katiba mpya nchi nzima.

Kauli hiyo ilitolewa jana na Mwenyekiti wa BAVICHA Taifa, John Pambalu, wakati akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam.

"Huu ni mwaka ambao tumejipanga kwa ajili ya kudai katiba mpya nchi nzima, tunafahamu kwamba jambo hili halitakuwa rahisi, lakini lazima tulifanye kwa maslahi ya vizazi vinavyokuja," alisema Pambalu.

Suala wanalokusudia kulifanya mwaka huu ni kumchagua Katibu Mkuu mpya wa Baraza hilo baada ya aliyekuwa akishikilia nafasi hiyo, Nusrat Hanje, kuvuliwa uanachama pamoja na wadhifa huo.

Nuzrat ni miongoni mwa wabunge 19 kutoka katika chama hicho ambao wamevuliwa uanachama baada ya kuapishwa kuwa wabunge wa viti maalum.

Pambalu pia aliikumbusha serikali kuhusu kuwafikiria vijana ambao wamehitimu vyuo vikuu na hawana ajira.

"Mwaka 2020 nao ulikuwa na changamoto kubwa ya vijana wengi wanaohitimu vyuo vikuu kukosa ajira, niikumbushe serikali kama ambavyo iliahidi kuwapatia ajira, ifanye hivyo," alisema mwenyekiti wa BAVICHA.

Aliwaambia wanahabari kuwa mwaka uliopita haukuwa mzuri katika masuala ya haki za binadamu na utawala bora hususani kwa baadhi ya viongozi kuacha kutumia sheria na kuamua kujichukulia sheria mkononi kwa kuwachapa viboko wakosaji.

"Mwaka jana ulikuwa na vituko, tumeshuhudia baadhi ya viongozi akiwamo Mkuu wa Wilaya ya Arusha ambaye badala ya kutumia sheria kwa wanafunzi waliofanya makosa, aliamua kuwachapa fimbo. Tukio hilo pia tumelishuhudia juzi kwa Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu anayeshughulikia Wenye Ulemavu, Ummy Nderiananga, haya ni mambo ya kushangaza," alisema Pambalu.

"Viongozi 'kunyuka' viboko watu bila kujali sheria ni kurudisha nchi enzi za ukoloni, alianza mkuu wa wilaya, lakini juzi tumeshuhudia tena kwa Naibu Waziri," alisema kiongozi huyo.

Aliiomba serikali iwaachie huru vijana wote waliokamatwa kutokana na uchaguzi mkuu mwaka jana.

"Matukio mengine ambayo yalitokea mwaka jana ni pamoja na vijana wengi kukamatwa, tunaomba serikali iwaachie wafungwa wanaotokana na uchaguzi wa mwaka 2020," alisema Pambalu.




Mkuu wa Wilaya ya Dodoma, Josephat Maganga (kulia), akimkabidhi funguo ya gari, William Mpachila mkazi wa eneo la Ipagala jijini Dodoma, juzi, ambaye alikuwa mshindi wa shindano la Shangwe Shangwena linaloendeshwa na kampuni ya Vodacom Tanzania, katikati ni Meneja wa Vodacom Kanda ya Kati, Grace Chambua. **MPIGAPICHA WETU**

# TFRA yawajengea uwezo wazalisha mbolea

**Na Mwandishi Wetu**

WAZALISHAJI wa mbolea nchini wametakiwa kutumia fursa ya upatikanaji wa malighafi muhimu za kuzalisha mbolea kwa kuanzisha viwanda vya mbolea na visaidizi vyake, ili kukidhi mahitaji ya mbolea nchini.

Wito huo umetolewa na Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA), Dk. Stephan Ngailo, jijini Dodoma, wakati wa ufunguzi wa mafunzo ya kuwajengea uwezo wazalishaji wa mbolea nchini.

Dk. Ngailo alisema Tanzania ina akiba ya madini mbalimbali yakiwamo yanayotumika katika kuzalisha mbolea kama vile phospheti ambayo yanaongeza fursa kwenye uwekezaji wa kutengeneza mbolea na kumhakikishia mkulima uwapo wa mbolea bora za kutosha na kwa bei nafuu.

Alisema uzalishaji wa mbolea utasaidia kuongeza fursa za ajira kwa vijana na kupunguza kwa kiasi kikubwa changamoto ya ajira nchini.

Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya udhibiti wa mbolea, alisema kuwa viwanda vya mbolea na visaidizi vyake vinakidhi mahitaji ya mbolea kwa asilimia tano pekee ya mahitaji kwa mwaka ambayo ni tani 600,000.

Alisema hali hiyo inatokana na matatizo mbalimbali ikiwamo ukosefu wa taarifa muhimu na za kutosha kuhusu uzalishaji wa mbolea na visaidizi vyake na zinazohusiana na masuala ya uwekezaji.

Alisema uzalishaji wa ndani pia utaimarisha urari wa biashara na mataifa ya nje (Balance of Trade), utaongeza ajira na kupunguza ucheleweshaji wa upatikanaji wa mbolea na kuongeza pato la ndani.

Mafunzo hayo yaliyowaleta pamoja wazalishaji wa mbolea, wauzaji na watendaji mbalimbali wa serikali wanaohusika na masuala ya viwanda, uratibu wa uingizaji wa mbolea kutoka nje nchi na watumishi wa Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea nchini.

Vilevile Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania inatoa vibali vya utengenezaji, uagizaji na usambazaji nchini na kutoa miongozo mbalimbali ya usimamizi na udhibiti wa ubora na biashara ya mbolea.

## Mbunge kuipiga jeki kiuchumi UWT

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

MBUNGE wa Morogoro Mjini, Abdulaziz Abood, ameahidi kuusaidia Umoja wa Wanawake wa CCM (UWT), wilayani Morogoro Mjini kubuni mradi ya maendeleo ili kujiimarisha kiuchumi.

Abood, alisema hayo wakati akifungua Mkutano Mkuu wa viongozi wa matawi na kata wa UWT wa wilaya hiyo mwishoni mwa wiki.

Alisema wakati umefika kwa UWT wilayani humo kubuni miradi mipya na kuendeleza iliyopo kama zilivyo jumuiya nyingine za CCM na jambo hilo litapunguza utegemezi.

"Umefika wakati mbuni miradi ya kimaendeleo kupunguza kuomba misaada na zaidi kujiimarisha kiuchumi ili kuunga mkono kaulimbiu ya uchumi wa viwanda," alisema Abood.

Aliwaambia uchaguzi umekwisha kilichobakia ni viongozi kuweka nguvu moja kuwatumikia wananchi na kufanya vile walivyoahidi ili kutekeleza ilani ya CCM ya 2020-2025.

"CCM itaendelea kuaminiwa na wana Morogoro Mjini kama nguzo ya kupata majawabu ya uhakika kwa matatizo yanayowakabili, niwaombe viongozi wa jumuiya hii mshikamane, uchaguzi umekwisha..." alisema Abood.

Alisema atahakikisha jumuiya hizo zinakuwa na shughuli za kufanya kwa kubuni miradi mbalimbali kwa kushirikiana na viongozi wenzake kuwawezesha ili kuanzisha vikundi vya ujasiriamali na kuanzisha viwanda ambavyo vitatoa ajira.

Mwenyekiti wa UWT Wilaya ya Morogoro Mjini, Victoria Saduka, alisema jumuiya hiyo imejipanga kufanya siasa za uchumi na kupitia viongozi wataanzisha miradi na kutoa elimu ya ujasiriamali kwa wanachama wake itakayotoa fursa ya wao kujiajiri katika masuala ya ujasiriamali.

Katibu wa CCM Wilaya ya Morogoro Mjini, Sofia Kibaba, aliwataka viongozi walioshinda watekeleze kikamilifu ahadi zao ili kuwaletea wananchi maendeleo kwani kilichobakia sasa baada ya uchaguzi ni kuhakikisha jumuiya zinajengwa na kuongezewa nguvu ili zizidi kuimarika.

# Waliohusika mauaji Rais Kabila wapata msamaha

**Kinshasa,** DRC

WANAUME wawili waliopatikana na hatia ya mauaji ya Rais wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), Laurent Kabila, miaka 20 iliyopita, wamepewa msamaha.

Maofisa wawili wa ngazi ya juu wa aliyekuwa Rais Kabila, akiwamo Kanali Eddy Kapend na Georges Leta, walihusishwa na mauaji hayo.

Kabila, inadaiwa alipigwa risasi na mlinzi wake, ingawa walinzi hao wawili walipinga kuhusika na njama hiyo.

Rais Félix Tshisekedi alibadilisha hukumu ya kifo dhidi yao Juni, mwaka jana.

Hatua hiyo inajiri wakati kuna mvutano kati ya Rais Félix Tshisekedi na mtangulizi wake, Joseph Kabila ambaye ni mtoto wa Laurent Kabila.

**Awali kulikuwa na upokezanaji wa madaraka wa amani nchini humo, kwa takribani miaka 60 na wengi walipinga matokeo ya uchaguzi.**

Joseph Kabila alichukua madaraka baada ya kifo cha baba yake, mwaka 2001 na alitawala DRC kwa miaka 18, kabla ya Tshisekedi kushinda uchaguzi, Desemba mwaka 2018.

Awali kulikuwa na upokezanaji wa madaraka wa amani nchini humo, kwa takribani miaka 60 na wengi walipinga matokeo ya uchaguzi.

Kumekuwa na tuhuma kali kwamba rais huyo mpya alifanya makubaliano ya nyuma ya pazia na Joseph Kabila, ambaye bado ana ushawishi mkubwa nchini.

Ofisi ya Rais Tshisekedi, ilisema msamaha wa rais ulitolewa kwa kila mtu aliyehukumiwa kifungo cha miaka 20 gerezani na ambao walikuwa wametumikia vifungo vyao kufikia Desemba 31, mwaka jana.

Giscard Kusema, kutoka ofisi ya rais idara ya habari, aliliambia Shirika la Habari la AFP kwamba, Kanali Kapend na watuhumiwa wenzake wamenufaika na msamaha wa rais.

Kanali Kapend, alikuwa mtumishi wa karibu wa Laurent Kabila.

Pia, Kanali Kapend alipatikana na hatia ya kupanga mauaji pamoja na maofisa wengine kadhaa wa kitengo cha usalama cha marehemu Kabila, pamoja na mkuu wa upelelezi wa wakati huo Georges Leta.

Msamaha huo wa rais, umetolewa wiki chache baada ya Rais Tshisekedi kuvunja muungano wake na chama cha Kabila, kilicho na wabunge wengi baada ya kuongezeka kwa taharuki.

Rais huyo, sasa anatafuta washirika wapya watakaoungana naye ili apate wabunge wengi ndani ya bunge. **BBC**



Gari ambalo limesababisha vifo vya takribani watu 56 na kujeruhi wengine 20, nchini Niger. Shambulizi hilo, lilitokea juzi katika vijiji vya Tchomb-Bangou na Zaroumdareye vilivyo jirani na mpaka kati ya nchi hiyo na Mali. **PICHA: AP**

# Mlipuko wa gari waua wanajeshi

**Menaka,** MALI

WANAJESHI wawili wa Ufaransa wameuawa baada ya gari lao kugonga kifaa chenye mlipuko, wakati wa operesheni Kaskazini Mashariki mwa Mali, siku chache baada ya wengine watatu kuuawa katika tukio kama hilo.

Kwa mujibu wa maofisa wa jeshi, vifo vimefikia 50 vya wanajeshi wa Ufaransa waliouawa katika taifa hilo la Afrika Magharibi tangu mwaka 2013 wakati Ufaransa, ilipoamua kusaidia kurudisha nyuma vikosi vya jihadi.

Ujumbe wa ofisi ya Rais wa Ufaransa, Emmanuel Macron, ulisema, amepata huzuni kubwa baada ya tukio hilo, kufutia vifo vya Sajini Yvonne Huynh na Koplo Loic Risser, katika mkoa wa Menaka.

Huynh, (33) mwenye mtoto mdogo, alikuwa askari wa kwanza wa kike kuuawa tangu operesheni ya Ufaransa ilipoanza katika mkoa wa Sahel, pia Risser (24) ni kati ya wanajeshi wa kikosi maalumu cha ujasusi.

"Gari lao liligonga kifaa cha kulipuka wakiwa kazini," ujumbe wa rais wa Ufaransa ulisema kuhusu tukio hilo la Jumamosi.

Aidha, askari mwingine alijeruhiwa katika mlipuko huo ingawa majeraha hayakuwa ya kutishia maisha, iliongeza taarifa hiyo.

Kikosi cha Barkhane cha Ufaransa chenye wanajeshi 5,100 mjini Sahel, pamoja na wanajeshi kutoka Mauritania, Chad, Mali, Burkina Faso na Niger, ambao kwa pamoja wanaunda kundi la G5 Sahel. kinapambana na vikundi vya jihad.

Macron alithibitisha dhamira ya Ufaransa ya kufuata vita dhidi ya ugaidi baada ya mashambulio ya hivi karibuni ambayo yanakuja wakati Paris inazingatia kupunguza ukubwa wa vikosi Afrika.

Kikundi kinachohusishwa na Al-Qaeda kuunga mkono Uislamu na Waislamu (GSIM) kilidai kuhusika na shambulio la Jumatatu ambalo liliwaua wanajeshi watatu wa Ufaransa katikati mwa Jimbo la Sahel.

Watu 4,000 walifariki mwaka 2019 kutokana na ghasia za jihad na mizozo ya kikabila iliyosababishwa na Waislam Mali, Burkina Faso na Niger, kulingana na Umoja wa Mataifa (UN). **RFI**

## Maandamano kumpinga Netanyahu yaendelea Israel

**Jerusalem** ISRAEL

MAANDAMANO ya kumtaka Waziri Mkuu, Benjamin Netanyahu, ajiuzulu kwa sababu ya kesi ya ufisadi na kushindwa kwake kusimamia vizuri janga la corona, yameendelea nchini Israel.

Inaelezwa ni miezi nane sasa tangu kuanza kwa maandamano hayo.

Licha ya karantini ili kupambana na Covid-19, waandamanaji wengi walihudhuria maandamano hayo karibu na makazi ya Waziri Mkuu, huko Jerusalem Magharibi.

Waandamanaji walikuwa wamebeba mabango yakisema kila mtu ni sawa mbele ya sheria na wamemtaka Netanyahu, ajiuzulu.

Maandamano kama hayo yalifanyika katika sehemu tofauti za nchi, haswa huko Tel Aviv na pia Magharibi mwa Jerusalem.

Kwa upande mwingine, polisi wa Israel, waliwakamata waandamanaji nane kwenye maandamano mbele ya makazi ya Waziri Mkuu Oslo hapo jana.

Maandamano yamekuwa yakiendelea kwa wiki 28 huko Israel, yameathiriwa na janga la corona na ukosefu wa ajira unaongezeka pole pole.

Desemba 27, mwaka jana, utawala wa Netanyahu uliamua kuwaweka wananchi karantini, wiki mbili nchini kote kwa sababu ya kuongezeka kwa visa vya kila siku katika janga hilo. **TRT**

## 10 wafa maporomoko ya ardhi, maelfu wahamishwa

**Oslo,** NORWAY

IDADI ya waliopoteza maisha katika maporomoko ya ardhi yaliyotokea, Desemba 30 katika kijiji cha Gjerdrum, Norway, imeongezeka

Miili ya watu watatu imepatikana katika kijiji cha Gjerdrum, imefanya idadi kufikia vifo 10 baada ya maporomoko ya ardhi kilomita 40 kutoka mji mkuu Oslo.

Msemaji wa Polisi, Knut Hammer alisema kuwa juhudi za kutafuta na uokoaji zinaendelea kwa miili saba ambayo bado haijulikani ilipo.

Imetangazwa kuwa watu 10 wamejeruhiwa katika maporomoko ya ardhi yaliyotokea katika kijiji cha Gjerdrum.

Zaidi ya watu 1,000 walihamishwa kutoka eneo hilo. **TRT**

# POCHETTINO ACHIMBA MKWALA NYOTA PSG



**PARIS,** Ufaransa

MAURICIO Pochettino amekubali kwamba, yupo kwenye presha kubwa baada ya kuchukua mikoba ya kuinoa Paris Saint-Germain na amewaonya nyota wa klabu hiyo lazima wathibitishe wanastahili kuvaa jezi ya timu hiyo.

Kocha huyo mwenye umri wa miaka 48, alikuwa hana kazi tangu alipoondoka Tottenham Hotspur Novemba mwaka 2019, hatimaye alithibitishwa kuchukua mikoba ya Thomas Tuchel pale Parc des Princes, Jumamosi.

Kocha huyo wa zamani wa Spurs, Southampton na Espanyol, Pochettino amesaini mkataba na mabingwa hao wa Ligi Kuu Ufaransa, Ligue 1, hadi Juni 2022, huku kukiwamo na kipengele cha kuongeza mwaka mmoja zaidi.

Pochettino amerudi kwenye klabu ambayo alitumia misimu miwili na nusu akiwa mchezaji, ambapo alibeba taji la Intertoto msimu wa 2000-01.

PSG ina desturi ya kushinda mataji kila msimu na raia huyo wa Argentina analifahamu hilo na hivyo anatarajia ubora kutoka kwenye kikosi chake.

"Nina furaha kubwa hapa. Ni nafasi kubwa kwangu, mradi huu ni wa aina yake," alisema akiiambia tovuti ya klabu hiyo.

"Kuwa na uwezo wa kuisaidia Paris Saint-Germain kutwaa mataji, hapa litakuwa jambo jema zaidi.

# Madrid yamwinda Son

**MADRID,** Hispania

KLABU ya Real Madrid imeripotiwa kumfukuzia mshambuliaji wa Tottenham Hotspur, Son Heung-min.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Korea Kusini ametengeneza ushirikiano mzuri sana na Harry Kane msimu huu na tayari anajivunia mabao 15 na pasi za mwisho nane katika mashindano yote kwenye kikosi hicho cha Jose Mourinho.

Spurs inasemekana wanatarajia kumpa mkataba mpya kama jambo muhimu au dharura, na mkataba wake wa sasa unaisha mwishoni mwa msimu wa 2022-23.

Hata hivyo, mwandishi wa habari wa Uturuki, Ekrem Konur amedai kwamba, kocha wa Real Madrid, Zinedine Zidane anampenda Son na angependa kumleta mshambuliaji huyo pale Bernabeu msimu wa majira ya joto.

Konur ameongeza kuwa mabingwa hao wa LaLiga, hivi karibuni watawasiliana na wawakilishi wa Tottenham juu ya uwezekano wa kufanya makubaliano ya biashara hiyo, ingawa Mourinho ameonyesha matumaini juu ya kumbakiza Son kwenye vitabu vya Spurs.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 28, amefunga mabao 99 kwa Spurs tangu awasili kutoka Bayer Leverkusen katika msimu wa joto wa 2015.






# *Lampard: Havertz anahitaji muda*

**LONDON,** England

FRANK Lampard amesema Kai Havertz bila shaka yoyote anahitaji muda wa kuonyesha kipaji chake pale Chelsea baada ya kuanza kwa kusuasua.

Nyota huyo wa kimataifa wa Ujerumani amekuwa na wakati mgumu tangu alipotua hapo akitokea Bayer Leverkusen na kujiunga Chelsea kwa ada iliyoripotiwa kuwa pauni milioni 72, uhamisho uliokamilika Septemba mwaka jana.

Havertz amefunga bao moja na kutoa pasi ya mwisho moja kwenye mechi 14 za Ligi Kuu ya England na amekuwa akitokea benchi katika mechi tatu za Blues zilizopita.

Hata hivyo, Lampard amesisitiza mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 21 bado anahitaji muda zaidi kuweza kuwa kwenye ubora wake.

"Kai wakati anakuja hapa alikuwa kwenye kiwango bora kabisa, lakini kwa sasa kiwango chake si kile, ila naamini ataimarika tu," alisema Lampard.

"Nimeona vitu vichache katika siku za hivi karibuni, namna gani pia wanavyopitia wakati mgumu.

"Kwa sasa hayupo kwenye ubora wake, lakini naamini mambo yatabadilika kwa haraka na nimeshazungumza naye."

HABARI MICHEZO

# Sheffield yaweka rekodi ya kichapo EPL

**LONDON,** England

SHEFFIELD United imevunja rekodi mpya kwenye Ligi Kuu England, baada ya kuwa klabu ya kwanza kucheza mechi 17 bila kupata ushindi.

Sheffield walianza kwa kufikia rekodi ya Queens Park Rangers ya kucheza mechi 16 bila ushindi wakati wa mchezo dhidi ya Barley ambapo walichapwa bao 1-0.

Sasa timu hii, imepata rekodi mbaya zaidi baada ya kukamilisha mechi 17 bila kuchukua pointi tatu kwenye Ligi Kuu England, tangu Bolton Wanderers kuwa na rekodi ya mechi 22 bila ushindi msimu wa 1902-1903.

Rekodi hii si ya kujivunia kwa Sheffield ambao hadi sasa wamefanikiwa kupata pointi mbili tu tangu msimu unaanza wakiwa nafasi ya mwisho ya msimamo wa ligi kwa sasa.

Vijana hao wa kocha, Chris Wilder wapo kwenye hatari kubwa ya kushuka daraja mwishoni mwa msimu huu.






# ZIDANE AMGEUKIA BENZEMA, AMTAJA HAZARD

**PARIS,** Ufaransa

ZINEDINE Zidane hana mpango wa kumpumzisha straika wa Real Madrid, Karim Benzema wakati akiahidi kumrudisha polepole, Eden Hazard ili awe fiti.

Benzema alishindwa kupiga shuti lolote lililolenga goli wakati Madrid ikiibuka na ushindi wa mabao 2-0 dhidi ya Celta Vigo kwenye mchezo wa Ligi Kuu Hispania, LaLiga, Jumamosi.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 33, ameanza katika mechi 15 za Madrid kati ya 17 za LaLiga msimu huu na ni golikipa, Thibaut Courtois na Raphael Varane ndio waliocheza mechi nyingi zaidi yake.

Wakati alipoulizwa kwenye mkutano na waandishi wa habari baada ya mchezo huo kama Benzema, ambaye amefunga mabao nane kwenye LaLiga, anahitaji kupumzika, Zidane alikataa.

"Sidhani kama amechoka," alisema Zidane. "Nafikiri alifanya vizuri na nilimtoa nje kwa sababu mchezaji mwingine alitakiwa kucheza. Tupo kwenye msimu mzuri. Tunafanya vitu sahihi na tutaendelea kuwa hivyo."

Hazard aliingia akitokea benchi kwenye mchezo huo wakati akiwa kwenye harakati za kurudi kwenye ubora wake baada ya kusumbuliwa na majeraha ya mara kwa mara.

"Tunakwenda kidogo kidogo," aliongeza Zidane. "Kidogo kidogo, unatakiwa kubadilisha mtazamo na hisia.

# *Donnarumma atakiwa Chelsea*

**MILAN,** Italia

GOLIKIPA wa AC Milan, Gianluigi Donnarumma, ameanza mazungumzo na Chelsea ili kutua katika klabu hiyo wakati wa dirisha la majira ya joto.

Kwa mujibu wa mwandishi wa habari wa England, Simon Phillips, amedai kuwa klabu ya Chelsea imeanza mazungumzo na mlinda mlango huyo Donnarumma na wana matumaini ya kumvuta ajiunge klabuni hapo katika dirisha lijalo la usajili baada ya mkataba wake kumalizika.

Mkataba wa Donnarumma unaisha katika dirisha lijalo la majira ya joto na hadi sasa Milan hawajafanya mazungumzo ya mkataba mpya na kipa huyo.

Kulingana na vyombo mbalimbali vya habari za michezo, vinasema kipa huyo amepewa mkataba wenye thamani ya pauni milioni sita kwa mwaka.

Mchezaji huyo raia wa Italia anasimamiwa na wakala mkubwa duniani Mino Raiola, ambaye amekiri klabu nyingi zinamhitaji ikiwamo, Juventus na Inter Milan.



# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# ARTETA: SOKA SASA NI TAMBARARE ARSENAL

**Ni ushindi wa tatu mfululizo tulizungumza kuhusu umuhimu wa kushinda na kila kitu...**

**LONDON,** England

MIKEL Arteta anaamini Arsenal sasa inaweza kucheza kwa uhuru baada ya kupindua kiwango chao na kushinda mechi tatu mfululizo.

**'Washikabunduki' hao walishinda mchezo wao wa tatu wa Ligi Kuu England juzi Jumamosi baada ya kuwafunga West Bromwich Albion mabao 4-0 pale kwenye dimba la Hawthorns ambalo lilijaa mvua ya theruji.**

Mabao mawili ya Alexandre Lacazette ya kipindi cha pili yaliiwezesha Arsenal kupata ushindi wa mabao manne na kuwavuta hadi nafasi ya 11 kwenye msimamo, baada ya Kieran Tierney na Bukayo Saka kila mmoja kufunga moja na kuipa uongozi wa mapema.

Ushindi huo wa tatu mfululizo umewafanya Arsenal kumaliza kipindi kibaya cha kucheza mechi saba mfululizo bila ushindi na Arteta ana matumaini sasa mambo yamebadilika na wataendelea kushinda.

"Natumaini hivyo, angalau sasa timu inashawishi kwamba imebadilika na unaweza kupata matokeo katika kila mchezo, mambo yanaonyesha kuwa chanya sana kwa sasa," alisema Arteta akiwaambia waandishi wa habari mara baada ya mchezo huo.

"Mwisho wa siku, sikufirikia sana kuhusu kiwango cha wachezaji.

"Nafikiri tulipoteza mechi zetu kwa sababu tulikuwa hatuna bahati na mara nyingi ilikuwa ni kwa sababu yetu wenyewe kwa kufanya makosa na tukaadhibiwa.

"Lakini unahitaji kushinda mechi na sasa mambo yamekuja tofauti kabisa, ngumu tofauti, na sasa wameondoa breki na unaweza kuona kwamba wanacheza kwa uhuru zaidi."

Arteta anaamini kikosi chake kilikuwa bora zaidi licha ya mchezo huo kutawaliwa na mvua ya theluji na ana imani mambo yataendelea kuwa hivyo kwa mechi zijazo.

"Tulitawala mchezo na kwa uhakika kabisa ilinishawishi, na nina imani kubwa mambo yataendelea kuwa hivi," alisema kocha huyo raia wa Hispania.

"Ni ushindi wa tatu mfululizo ndani ya wiki. Tulizungumza kuhusu umuhimu wa kushinda na kila kitu sasa kimebadilika."

## ZISIKUPITE

### POCHETTINO NA MBAPPE

KOCHA mpya wa Paris St-Germain, Mauricio Pochettino, ana matumaini straika wa Ufaransa, Kylian Mbappe, mwenye umri wa miaka 22, atasaini mkataba mpya licha ya kuwaniwa na Liverpool. ***(AS)***

### POGBA SASA KUUZWA

MANCHESTER United itamuuza kiungo wa Ufaransa, Paul Pogba, mwenye umri wa miaka 27, kipindi cha majira ya joto kijacho baada ya kukubali kwamba hatasaini mkataba mpya. ***(Sunday Mirror)***

### INTER KUMTOA ERIKSEN

INTER Milan wametoa ofa kwa kiungo wa zamani wa Tottenham Hotspur, Christian Eriksen kwenda Real Madrid na Atletico Madrid. Raia huyo wa Denmark mwenye umri wa miaka 28, pia amekuwa akihusishwa na Paris St-Germain. ***(Marca)***

### UNITED YAMPOTEZEA SANCHO

MANCHESTER United haina uhakika kama itaweza kumshawishi winga wa England, Jadon Sancho mwenye umri wa miaka 20, huku kocha Ole Gunnar Solskjaer, akiwa anavutiwa zaidi na straika wa Borussia Dortmund na Norway, Erling Braut Haaland mwenye umri wa miaka 20. ***(Sunday Mirror)***

### DIALLO KUPELEKWA UNITED

KLABU ya Atalanta inataka kumtoa kwa mkopo winga wake, Amad Diallo mwenye umri wa miaka 18 raia wa Ivory Coast kwenda Manchester United kwa kipindi chote cha msimu kilichobaki. ***(Manchester Evening News)***

### SALIBA KUONDOKA ARSENAL

WILLIAM Saliba yupo tayari kupunguziwa mshahara ili aondoke Arsenal, huku klabu kadhaa zikionyesha nia ya kumwania mlinzi huyo mwenye umri wa miaka 19, wakati huu wa dirisha dogo la usajili. ***(L'Equipe via Sport Witness)***

### KABAK AGOMBEWA EPL

CRYSTAL Palace na Leicester ni miongoni mwa klabu zinazowania kumsajili mlinzi wa Schalke na Uturuki, Ozan Kabak mwenye umri wa miaka 20. ***(Mail on Sunday)***

### TOMORI HUYO NEWCASTLE

KOCHA wa Newcastle, Steve Bruce ana matumaini ya kumsajili kwa mkopo mlinzi wa Chelsea, Fikayo Tomori mwenye umri wa miaka 23. ***(Mail on Sunday)***

### GIROUD ANOGEWA CHELSEA

MSHAMBULIAJI wa Ufaransa, Olivier Giroud mwenye umri wa miaka 34, ambaye amekuwa akihusishwa na West Ham amesema angependa kubaki Chelsea na kushinda mataji. ***(Sky Sports)***

### FOSU-MENSAH KUBAKI UNITED

TIMOTHY Fosu-Mensah, 23, anataka kubakia Manchester United licha ya hivi karibuni kukataa kusaini mkataba mpya. ***(Manchester Evening News)***

HABARI MICHEZO

## KMKM yaanza nyodo kileleni

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

HUKU wakiendelea kujiimarisha kileleni mwa msimamo wa Ligi Kuu Zanzibar, Kocha Mkuu wa timu ya KMKM, Ame Msimu, amesema lengo lake ni kuhakikisha wanautwaa ubingwa wa ligi hiyo baada ya kuukosa msimu uliopita.

Hadi sasa KMKM ipo kileleni mwa msimamo wa Ligi Kuu Zanzibar ikiwa na pointi 19 baada ya kushuka dimbani mara nane ikishinda mechi sita, sare moja na kupoteza moja.

Akizungumza na gazeti hili juzi, Msimu alisema kufanya vizuri kwa KMKM katika mzunguko huu wa kwanza ambao umebakisha mechi tatu kabla ya kumalizika kunatokana na wachezaji wake kujituma na kufuata vema maelekezo yake.

Alisema bado yapo makosa madogo madogo yanayofanywa na safu ya ulinzi na ushambuliaji hali inayosababisha kushindwa kupata mabao mengi, hivyo hilo linahitaji kufanyiwa kazi kubwa.

Katika msimamo wa ligi hiyo, timu ya Black Sailor inashika nafasi ya pili ikiwa na alama 14 baada ya juzi kutoka na ushindi wa mabao 2-0 dhidi ya Mafunzo, huku Maafande wa Zimamoto wenye alama 12 wakishika nafasi ya tatu baada ya juzi nao kuibuka na ushindi wa mabao 2-1 dhidi ya Mlandege.

## Nusu fainali Mapinduzi Cup wanawake kesho

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

TIMU ya New Generations na Jumbi Queens kutoka Kundi A la michuano ya Kombe la Mapinduzi kwa upande wa wanawake, zimetinga hatua ya nusu fainali.

Aidha, kwa upande wa Kundi B timu ya New Sisters nayo imeungana na Future Queens kutinga hatua hiyo ya nusu fainali inayotarajiwa kuchezwa kesho.

Akizungumza na gazeti hili juzi, Mwenyekiti wa Kamati ya Soka la Wanawake (ZFF), Nasra Juma, alisema kesho zitachezwa nusu fainali mbili katika Uwanja wa Mao B, huku nusu fainali moja ikichezwa majira ya saa nane mchana na ya pili saa 10 alasiri.

Alisema mashindano hayo licha ya kuanzishwa kwa mara ya kwanza mwaka huu, yamefanikiwa kwa kiasi kikubwa kwa upande wa timu zote zilizoshiriki michuano hiyo licha ya changamoto ndogo ndogo hususan timu mpya.

Alisema timu za wanawake zinakabiliwa na changamoto ya vifaa vya michezo ikiwamo jezi, viatu, mipira pamoja na vifaa vingine vya mazoezi.

Timu zilizoshiriki mashindano haya ya Kombe la Mapinduzi ni tisa ambazo ni New Generations, Women's fighters, Green Queens, Jumbi Queens, Future Queens, New Sisters, Ladies Fighters, Amaan Queens na Yellow Queens huku timu moja kutoka kisiwani Pemba ya mkoani Queens ikishindwa kushiriki mashindano haya kutokana na changamoto ya fedha.

# NAMUNGO YAWAFUATA WASUDAN MAJEMBE 18

**Na Shufaa Lyimo**

WAWAKILISHI wa Tanzania kwenye Kombe la Shirikisho barani Afrika, Namungo FC, jana wamekwea pipa kuelekea Sudan wakiwa na majembe yao ya kazi 18, tayari kwa mechi hiyo ya marudiano dhidi ya wenyeji wao, El Hilal Obeid itakayopigwa keshokutwa, Jumatano, imeelezwa.

Namungo itashuka dimbani nchini Sudan Jumatano, tayari ikiwa na faida ya mabao mawili baada ya kushinda 2-0 kwenye mechi ya awali iliyopigwa Uwanja wa Azam Complex, Chamazi jijini Dar es Salaam, hivyo inahitaji sare ama ushindi wowote au kutokubali kupoteza kwa zaidi ya bao 1-0.

Akizungumza jijini jana, Katibu Mkuu wa Namungo FC, Ally Selemani, alisema timu hiyo imewakosa wachezaji wake watano na imeondoka na msafara wa watu 29 ambapo kati yao viongozi wapo 11 na wachezaji 18.

**Katibu huyo aliwataja wachezaji hao ambao hawakuambatana na timu kuwa ni nahodha Hamis Fakhi, Adam Salamba, Lucas Chamboja pamoja na Abdulhamid Humud ambao ni majeruhi.**

"Timu itaondoka leo (jana) saa 11:000 jioni kuelekea Sudan, maandalizi yanaendelea vizuri kuelekea katika mchezo wetu," alisema Selemani.

Aidha, aliwaomba Watanzania kuendelea kuiombea timu hiyo ili iweze kuibuka na ushindi na kusonga mbele.

Alisema licha ya kuwa na wachezaji 24, kocha mkuu wa klabu hiyo, Hemed Morocco, amesikitika kuwakosa wachezaji hao ambao wana umuhimu mkubwa ndani ya timu.

Kuhusu usajili, alisema tayari wamepokea ripoti ya kocha na kwamba imeeleza anahitaji kuongeza wachezaji wanne, ambapo zoezi hilo atalifanya baada ya kurudi kutoka nchini humo.

Naye nahodha wa timu hiyo, Hamis Fakhi, alisema amesikitika kuukosa mchezo huo wa Kombe la Shirikisho huku akiwataka wachezaji wenzake kuzidi kushirikiana.

Alisema ni mchezo mgumu na muhimu kwao kushinda, lakini anaamini wachezaji waliosafiri watawawakilisha vizuri.




Wachezaji wa timu ya Chanika City wakiwa mazoezini kwenye Uwanja wa Shule ya Msingi Nguvukazi Chanika jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# *Kaseja na simulizi shabiki kumpora taulo*

**Na Adam Fungamwango**

KIPA wa KMC FC, Juma Kaseja, amesema amenusurika kuingia katika deni, baada ya shabiki mmoja wa Mbeya City kuingia uwanjani akitaka kuchukua taulo ambalo alikuwa ameliweka golini kwa ajili ya matumizi ya kujifuta maji kutokana na mvua zinazoendelea kunyesha maeneo mbalimbali nchini kwa sasa.

Kipa huyo wa timu ya Taifa ya Tanzania, Taifa Stars, akitoa simulizi hiyo, alianza kwa kueleza kwamba ilikuwa dakika ya 79, shabiki mmoja wa Mbeya City alipoingia uwanjani akitaka kwenda kuchukua taulo lililokuwa golini kwa kile alichoamini ni hofu ya imani za kishirikina, akidhani kuwa ndilo linalosababisha wachezaji wa timu hiyo kukosa mabao, lakini hata hivyo alidhibitiwa.

Tukio hilo la aina yake lilitokea Jumamosi kwenye Uwanja wa Sokoine jijini Mbeya, kwenye mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara, timu hizo zikitoka suhulu bila kufungana.

"Lile lilikuwa taulo la hoteli. Wala halikuwa na lolote lile wanalofikiria. Nililiomba hotelini kwa ajili ya mvua. Umeona mazingira ya mvua, tumecheza huku inanyesha, uwanja umeloa, nilikuwa nalitumia kujifutia glovu ili zikauke na mimi mwenyewe najifuta usoni, na kama shabiki huyo angefanikiwa kulichukua basi ningedaiwa, ningekuwa nimeshaingia demi kwenye hoteli tuliyofikia," alisema golikipa huyo mkongwe nchini.


Akionekana kushangazwa na tukio hilo, kipa huyo alisema magolikipa wengi huingia na taulo kwa ajili ya kujifutia jasho, lakini anashangaa taulo hilo kuhusishwa na ushirikina.

Miaka kadhaa nyuma, kipa mwingine aliyekuwa akipata sana misukosuko kutokana na taulo lake kuhisiwa vibaya na mashabiki ni Ivo Mapunda wakati akiitumikia timu ya Simba.

Staili hiyo ambayo aliipata akiwa Gor Mahia ya Kenya ambako hata huko alikuwa akipata kashikashi, alirejea nayo nchini akiwa na kikosi hicho na mara kwa mara mashabiki walikuwa wakiingia uwanjani wakitaka kulipora na hata baadhi ya waamuzi nao walikuwa hawakubali kuliona likiwekwa ndani ya lango.

# Michezo

Jumatatu Januari 4, 2021
Nipashe



Arteta: Soka ni tambarare Arsenal UKURASA 22

UTAMU KOLEA...



Wachezaji wa Arsenal wakimpongeza Alexandre Lacazette baada ya kuifungia timu hiyo bao la nne wakati wakishinda 4-0 kwenye mechi ya Ligi Kuu England dhidi ya West Bromwich Albion iliyopigwa Uwanja wa The Hawthorns juzi. Mabao mengine yalifungwa na Kieran Tierney, Bukayo Saka na Lacazette mawili. PICHA: MTANDAO

## Yanga sasa yafuata Kombe la Mapinduzi

**Na Shufaa Lyimo**

BAADA ya kuhitimisha raundi ya kwanza ya Ligi Kuu Bara ikiwa kileleni mwa msimamo, leo Yanga itaelekea visiwani Zanzibar tayari kuanza mbio za kusaka ubingwa wa Kombe la Mapinduzi ambayo itaanza kesho.

Yanga ambayo kwenye michuano hiyo ipo Kundi A pamoja na Namungo na Jamhuri ya Pemba, itashuka katika Uwanja wa Amaan kesho saa 2:15 usiku kutupa karata yake ya kwanza dhidi ya Wapemba hao.

Timu zingine zinazoshiriki michuano hiyo ni Simba, mabingwa watetezi Mtibwa Sugar na Chipukizi ya Pemba ambazo zipo Kundi B, huku Kundi C likiundwa na Azam FC, Malindi na Mlandege.

Akizungumza na gazeti hili jijini Dar es Salaam jana, Makamu Mwenyekiti wa Klabu ya Yanga, Fredrick Mwakalebela, alisema lengo lao mwaka huu ni kutwaa kombe hilo linaloshikiliwa na Mtibwa Sugar.

"Tutaondoka kesho (leo) kuelekea Zanzibar kushiriki mashindano ya Kombe la Mapinduzi, tutaendeleza ushindani ule ule kama tulivyofanya kwenye Ligi Kuu," alisema Mwakalebela.

Alisema Kocha Mkuu, Cedric Kaze, amekiandaa vema kikosi chake kupata matokeo mazuri katika mashindano hayo na kwamba ushindani uliopo wa namba ndani ya timu yao ni wa kuvutia.

# Mugalu mbeleko Simba kwa Platinum

## ● ● ● Sven asema wapo tayari, rekodi ya kufunga ya Chikwende yatisha, lakini...

**Na Mwandishi Wetu**

WAKATI mabeki wa Simba tayari wanajua hawapaswi kufanya makosa ya kumkaba winga 'teleza' wa FC Platinum, Perfect Chikwende, ambaye aliwaadhibu katika mechi ya kwanza ugenini ya Ligi ya Mabingwa Afrika, kwa upande wao mshambuliaji Chris Mugalu, anatarajiwa kubebeshwa 'makombara'ya kuwaadhibu 'wajukuu' hao wa Robert Mugabe, imefahamika.

**Simba itaikaribisha FC Platinum keshokutwa, Jumatano katika Uwanja wa Benjamin Mkapa baada ya kukubali kipigo cha bao 1-0 ugenini, shukrani zikimwendea 'muuaji' Chikwende aliyewazamisha 'Wekundu wa Msimbazi' hao kwenye mechi hiyo ya awali.**

Lakini Kocha Mkuu wa Simba, Sven Vandenbroeck, amesema hana wasiwasi kuhusu kikosi chake kupindua matokeo Jumatano, huku taarifa za klabu hiyo zikimwelezea Mugalu kama mmoja wa washambuliaji ambaye hana utani langoni na kwamba anachojua ni kufunga tu na kuwapa raha mashabiki wa klabu hiyo.

"Yeye anajua kufunga tu na kuwapa furaha Wanasimba. Tarehe 6 Januari 2021 (Jumatano), ana kazi maalumu ya kuwamaliza 'wajukuu' wa Mugabe. Wanasimba tujitokeze kwa wingi kuishangilia timu yetu," ilieleza taarifa ya Simba.

Katika mechi iliyopita ambayo ilipigwa Uwanja wa Taifa wa Zimbabwe, Mugalu aliingia akitokea benchi kipindi cha pili kuchukua nafasi ya Meddie Kagere, na kufunga bao, lakini tayari mshika kibendera alishaonyesha kuwa mfungaji alikuwa ameotea.

Na katika mechi mbili zilizopita dhidi ya Majimaji kwenye Kombe la FC na Ihefu FC kwenye Ligi Kuu Bara, zote Mugalu alitokea benchi na kufunga bao wakati Simba ikishinda mabao 5-0 na 4-0.

Akizungumzia mchezo huo, Sven alisema wamejiandaa kutumia vema dakika 90 za pili zilizobaki na hawatafanya makosa waliyofanya nyumbani katika mechi hiyo.

Alisema wanaendelea na mazoezi na wamejipanga vizuri kuelekea mchezo huo ambao anaamini utakuwa mgumu kwa timu zote, hasa ukizingatiwa tayari wapinzani wao wapo mbele kwa bao moja.

"Tuliadhibiwa kutokana na makosa tuliyofanya, lakini sasa tumeyafanyia kazi na tunaendelea kuyafanyia kazi, naamini tutakuwa katika kiwango bora na tutawapa furaha mashabiki wetu," alisema kocha huyo raia wa Ubelgiji.

Simba ambayo ilitinga hatua hiyo baada ya kuitoa Plateau United ya Nigeria kwa kuwafunga bao 1-0, likizamishwa nyavuni na Clatous Chama, itahitaji ushindi kuanzia mabao 2-0 dhidi ya Platinum ili kuitoa na kutinga hatua ya makundi.

Hata hivyo, haitakuwa rahisi kutokana na rekodi nzuri ya FC Platinum ikiwa ugenini, kwani ilitinga hatua hiyo baada ya kushinda ugenini na nyumbani dhidi ya Costa do Sol ya Msumbiji kwa mabao 2-1 mjini Maputo na ziliporudiana Harare ikashinda 2-0.

Katika mechi hizo tatu za Ligi ya Mabingwa hadi sasa, mbili dhidi ya Costa do Sol na moja dhidi ya Simba, zote Chikwende alicheka na nyavu, hivyo ni mmoja kati ya wachezaji ambao mabeki wa Simba wanapaswa kumchunga zaidi.

9 770856 541002 >

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042